
# Fikiri Riziki!

**Huu ni mwongozo wa mafunzo ya Lenzi ya Riziki, mwongozo huu unaelezea jinsi ya kuutumia kwa watu, kaya ama jamii iliyoathiriwa na ugonjwa wa Ukimwi**



*Fikiri Riziki!* Ni mwongozo ulioandikwa kwa pamoja na Tearfund na Samaritan's Purse

# Fikiri Riziki!

**Huu ni mwongozo wa mafunzo ya Lenzi ya Riziki kwa wawezeshi, mwongozo huu unaelezea jinsi ya kuutumia kwa watu, kaya au jamii zilizoathiriwa na ugonjwa wa Ukimwi.**

Tafsiriwa kutoka **Think Livelihoods!**

Tearfund pamoja na Samaritan's Purse UK

Waandishi: Kara Greeblott, Isabel Carter na Debora Randall

Picha ya Mwanzo: Moses Kamau Wanjiru

Michoro na vielelezo: Rod Mill, Amy Levene na Steve Pickering

Tafsiri: Moses Kamau Wanjiru

Muundo: Wingfinger Graphics

Mwongozo huu umejaribiwa, ukapitiwa upya kwa msaada wa watu wafuatao ambao ni wafanya kazi na marafiki kutoka Tearfund na Samaritan's Purse;

Ephraim Kahsay, Moses Kamau Wanjiru, Jimmy Francis Odongo, Emmanuel Oboi, Sileshi Tegegne, Hailemicael Chane, Bitsuaamlak G/Ab, Yideneku Melese, Desalegn Demisse, Tamene Tessema, Etagegn Gudebo, Alula Debela, Tewodros Belachew na Lilian Adong.

Sheheni kiingereza asilia © 2011 Tearfund na Samaritan's Purse UK

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuchapisha au kunakili sehemu yeyote ya kitabu hiki bila idhini ya mhusika.

Mwongozo huu umeandaliwa na mashirika mawili ya Kidini kwa lengo la kusaidia wadau mbalimbali wa makanisa wanaoshughulika na kazi ya kupambana na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi katika kutekeleza Lenzi hii, Hata hivyo, Mwongozo huu waweza kutumiwa na mashirika au wadau wengine pia

Tearfund ni shirika la Kiinjilisti la kikristo na pia la Maendeleo ambalo hufanya kazi kwa pamoja na mashirika mengine ya kidini na na ya kijamii katika kupamba na na umasikini.

Samaritan's Purse ni Shirika la kikristo lisilozingatia faida, linalotoa msaada na kujenga uwezo kwa makanisa na kusaidia shughuli za maendeleo, pia hutoamsaada kwa wahitaji ulimwenguni kote.

# Fikiri Riziki!

**Huu ni mwongozo wa mafunzo ya Lenzi ya Riziki kwa wawezeshi, mwongozo huu unaelezea jinsi ya kuutumia kwa watu, kaya au jamii zilizoathiriwa na ugonjwa wa Ukimwi**

## Yaliyomo


| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Utangulizi | 3 |
| | | Lengo la mwongozo huu | 5 |
| SOMO LA KWANZA | **1** | Maelezo ya jumla | 8 |
| SOMO LA PILI | **2** | Kutambua Rasilimali | 15 |
| SOMO LA TATU | **3** | Kuelewa mazingira magumu na jinsi ya kuyakabili | 22 |
| SOMO LA NNE | **4** | Taasisi, sera na michakato ya sera | 31 |
| SOMO LA TANO | **5** | Uchambuzi wa mzunguko wa thamani | 40 |
| SOMO LA SITA | **6** | Mikakati ya maisha | 47 |
| SOMO LA SABA | **7** | Kuchukua hatua | 53 |
| SOMO LA NANE | **8** | Kuiga na kufuatilia | 62 |


### Sehemu ya ziada/nyongeza


Sehemu ya Ziada A: Masomo ya Bibilia 64

Sehemu ya Ziada B: Masomo zaidi 70

Sehemu ya Ziada C: Michoro ya rasilimali 71

# Ufupisho wa maneno

| | |
|---|---|
| AIDS | Ukosefu wa kinga mwilini |
| ART/ ARV | Madawa ya kupunguza makali ya virusi vya Ukimwi |
| FBO | Mashirika ya kidini |
| HBC | Huduma ya nyumbani |
| HH | Kaya ama aila |
| HIV | Virusi vinavyosababisha Ukosefu wa kinga mwilini |
| KHC | Kanisa la Kale Heywet |
| M & E | Ufuatiliaji na Utathmini |
| MFI | Taasisi ndogondogo za kifedha |
| NGO | Mashirika yasiyo ya kiserikali |
| OVC | Watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi |
| PIPS | Sera, Taasisi, na Michakato |
| PLA | Mbinu shirikishi za masomo |
| PLHIV | Watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi |
| SHG | Makundi ya kusaidiana |
| TB | Kifua kikuu |
| VVU | Virusi vya Ukimwi |
| WKHC | Kanisa la Wolaitta Kale Heywet |

**Tafadhali kumbuka kuwa majina yote katika mwongozo huu, yaliotumika katika tafiti na yale yaliyonakiliwa yamebadilishwa kwa sababu za usiri.**

# Utangulizi wa lenzi ya maisha

Lengo la mwongozo huu ni kusaidia jamii na mashirika yasio ya kiserikali ambayo yanafanya kazi ya kupambana na ukimwi, kutekeleza “Lenzi ya riziki” kusaidia utenda kazi wao.

**“RIZIKI”** ni neno linalogusia shughuli zote za kimaisha zinazowezesha watu kukidhi mahitaji yao na kusaidia familia zao. Iinahusisha shughuli mbalimbali kama vile malipo baada ya kazi, mshahara, Upandaji wa mimea au ufugaji, uwezo wa kupika, useremala au ujuzi na biashara ndogo ndogo kama vile, kuwa na soko, ususi, au kutengeneza na kusindika vyakula.

**“LENZI”** Ni kipande cha Kioo au vioo ambavyo huvuta karibu, hukuza au Kupunguza ukubwa wa vitu machoni. Kulingana na mwongozo huu, ni njia ya kutazama ulimwengu .Hivyo basi, mwongozo huu wa Lenzi ya maisha/ Riziki, utasaidia watu kuangalia kwa makini na ufahamu jinsi wanavyoweza kusaidiana wenyewe na familia zao, maisha ya sasa na baadae.



*Kuanzisha biashara ndogondogo ni mbinu moja ya kujiendeleza kimaisha na inahitaji rasilimali kidogo (Picha: Moses Kamau Wanjiru / Samaritan’s Purse)*

### Kufanya kazi kwa pamoja kwa ufanisi

Biblia inazungumzia jinsi mwili wa binadamu ulivyo na sehemu tofauti. Ili jamii iweze kufanikiwa, ni lazima kuwepo na mgawanyo wa majukumu lakini pia kufanya kazi kwa umoja na wala si kwa ubinafsi. Watu katika jamii maskini wanahitaji kuwezeshwa namna ya kutumia vipawa na talanta walizonazo ili waweze kujikwamua kutoka kwa umasikini na kuongeza pato la familia yao na jamii yote kwa ujumla.

Kuna uhusiano wa karibu sana kati ya Ugonjwa wa Ukimwi na riziki. Maambukizi ya Virusi vya Ukimwi huathiri uwezo wa mtu wa kufanyakazi na kujishughulisha na shughuli zingine za kimaisha. Hii hupelekea wengine kubadilisha makazi yao na namna ya kujihusisha kijamii. Mambo mengi hubadilika na kuwafanya watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi kutafuta njia zingine za kujiendeleza kimaisha. Ni jambo la msaada sana iwapo watu hawa wataweza kutazama maisha yao kupitia mtazamo wa kijitabu hiki na kuweza kugundua fursa zingine za kujiendeleza. Hata hivyo, lenzi hii inaweza pia ikatumika katika muktadha/Hali tofauti na sio tu katika jamii zilizoathiriwa na ugonjwa wa Ukimwi.

Mwongozo huu unalenga kuandaa Wawezeshaji kutumia mbinu shirikishi kwa wahusika ili:

- Kupata uelewa wa pamoja wa hali ya jamii katika maeneo yao wanayoishi
- Kubadilishana uzoefu kuhusu mwongozo huu na jamii zilizolengwa
- Kuandaa na kuwapa uwezo familia, makundi maalumu katika na jamii kwa ujumla, kubaini fursa na kuamua hali bora ya maisha yao ya sasa na baadaye.

Kutumia mwongozo huu wa lenzi ya riziki, kutasaidia mashirika, makanisa na viongozi wa jamii:

- Kutimiza malengo yao kwa ufanisi
- Kuleta uendelevu zaidi kwa kazi inayohusiana na virusi vya ukimwi (VVU)
- Kuwa rahisi kubadilika katika kukabiliana na mabadiliko ya nje
- Kukabiliana kwa ufanisi kwa matakwa yote ya wadau katika ngazi zote (Serikali ya kitaifa, viongozi wa maeneo na wanafamilia)
- Kujenga nguvu zilizopo za walengwa, na kuwasaidia kuwa na uwezo zaidi wa kukabiliana na majanga na migogoro ya baadaye

> *“Mwongozo huu ni kama Twiga – unasaidia watu kufikia malengo ya juu na kupokea rasilimali ambazo hazingefikika hapo awali”*

Mwezeshaji wa mwongozo huu

Makanisa na mashirika mengi ya kidini yamewajibika kibibilia katika kutunza waliowanyonge na waliodhulumiwa. Wajibu huu umehimiza kanisa katika kujitoa kwa haki kuhudumia jamii na kuheshimu utu wa makundi yaliyoko pembezoni, yakiwemo yale yaliyo athiriwa na ugonjwa wa Ukimwi. Kwa mara nyingi, makundi ya kidini huwafikia watu waliotengwa na kukataliwa. Watu huyaamini sana mashirika ya kidini hasa wakati wa matatizo.

*"Watu wanajihusisha na biashara tofauti; Macho yao yamefunguliwa upya. Wameamshwa. Na sasa wako na uhusiano mzuri na wengine"*

Aliyenufaka kwa mafundisho haya

Mashirika ya kidini na makanisa yamechangia kwa kiasi kikubwa katika kuwasaidia na kuwatunza watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi kwa huruma na upendo. Mara nyingi, mashirika haya ya kidini na makanisa kwa ujumla huhusika kwa kutoa misaada ya kijamii na huduma zingine rasmi kwa lengo la kuwasaidia wahanga na watu wenye shida.

Mwongozo huu unaanza na imani kwamba Mungu ameweka ujuzi na rasilimali katika kila jamii. Makanisa na mashirika ya kidini yanaweza kuisaidia jamii kutambua na kutumia rasilimali hizo kujiletea maendeleo endelevu.

Lenzi hii ya riziki, pia itasaidia makanisa na mashirika ya kidini kutumia mbinu shirikishi zinazo wapa uwezo wa kutunza na kutoa misaada kwa wahitaji au wanyonge na kuwajengea uwezo ili waweze kuwajibika wenyewe na kujiletea maendeleo. Mwongozo huu utawezesha utaratibu, wa kusaidia watu katika jamii maskini kuongeza kipato na kukidhi mahitaji yao ya msingi kwa njia endelevu na ya kudumu, wakati huo huo kuwapa fursa ya kuishi kwa heshima katika mazingira ya haki na amani.

*"Sasa mmetupa changamoto ya kubadilisha mtazamo wetu kwa kutambua rasilimali zetu"*

Kanisa la Injili, Uhabeshi

## Kubadilisha tabia na mitazamo ya jamii

Kaskazini mwa nchi ya Uhabeshi, makanisa ya kiprotestanti yaliojitenga yamepitia mateso (Persecution) mengi kwa takriban miaka arobaini, makanisa haya yamekataliwa na jamii nzima. Jamii haikutarajia jambo zuri kutoka kwa kanisa, iliwatazama tu kama dhehebu, linaloendeleza uvivu na umasikini. Walilalamika kwamba kanisa lilizungumzia tu mambo ya kiroho pekee.

Kanisa la full Gospel, liliyatoa mafundisho haya ya riziki kwa kuwalenga watu tofauti katika miji miwili, Debre Markos na Injibara. Waliohusika ni kama vile Maafisa wa serikali, viongozi wa makanisa, viongozi wa kiislamu, makundi ya kujitegemea, wazee wa vijiji na viongozi wa mashirika yanayopambana na Ukimwi.

Jamii hizi sasa zimefahamu vyema lengo kuu la kanisa; "Sasa tunawaona mkija na mbinu mpya zinazolenga uwezo wetu wa kifedha na kutuwezesha kutumia rasilimali zetu vizuri. Mafundisho haya yamebadilisha matarajio yetu, hapo awali, tulijiona kuwa maskini. Tulitarajia msaada kutoka nje ili kutatua shida zetu, lakini sasa, baada ya mafundisho, tunajiona matajiri na tunauwezo wa kusuluhisha matatizo yetu."

Matokeo mengine ni kwamba baada ya mafundisho, ushirikiano baina ya dini tofauti ulibuniwa. Wanachama sabini tayari wamejiandikisha. Nia yao ni kusaidia watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi.



*Watu wengi wanaweza kuanzisha biashara ndogondogo hapo nyumbani (Picha: Moses Kamau Wanjiru / Samaritan's Purse)*

# Lengo la Mwongozo huu

Mwongozo huu unaazimia kuelezea moja kwa moja , kuelekeza na kusaidia kuelewa kwa vipengele tofauti vya mafundisho haya. Hii ni mbinu inayo saidia watu kuelewa rasilimali zao vizuri ili waweze kuzitumia na kujenga maisha dhabiti. Pia, utasaidia watu kuelewa mambo yanayowaweka hatarini na jinsi wanvyoweza kutumia mifumo na taratibu zilizopo kuboresha maisha yao.



*Wafanyi kazi katika miradi ya kushughulikia maambukizi ya ukimwi kwa mara nyingi watatumika kama wawezeshi wa mafundisho haya. (Picha: Moses Kamau Wanjiru / Samaritan's Purse)*

Mwongozo huu unaanza na maelezo ya jumla kuhusu mbinu hii ya mtazamo wa riziki. (**Sehemu ya 1** katika ukurasa 8), umeundwa kama njia ya kuutambulisha kwa mashirika, maafisa na viongozi wa jamii au Kanisa. Hii itaongeza ufahamu wa manufaa yaliopo katika kutumia mwongozo huu wa riziki vyema. Mara tu watakapoelewa, mashirika na viongozi mbali mbali katika jamii na kanisa wataweza kuchagua watu ambao watanufaika katika mafundisho haya. **Sehemu ya 1** yaweza kutumika katika kutambulisha mwongozo huu kwa waliochaguliwa kufundishwa.

Mwongozo huu umegawanyika katika sehemu tofauti, na kila sehemu yaweza kutumika na kufundishwa kivyake, au kwa pamoja katika darasa au mafunzo ya semina. Mbinu ya mafundisho yapaswa kushirikisha wahusika na kuhimiza vitendoshughuli (utekelezaji wake) Kila sehemu inajenga mafundisho ya sehemu zilizotangulia, lakini inawezekana kupanga sehemu hizi kwa njia ambayo itakayofaa mahitaji ya ndani. Uzoefu unaonyesha ya kwamba ni vyema kuwaleta watu pamoja ili kujifunza sehemu moja au mbili kwa wakati mmoja, ambapo huwasaidia kuelewa kwa kina na baadaye kwenda kuyafanyia kazi mafundisho hayo kabla ya kurejelea tena.

Kuna vifungu vingi vya bibilia ambavyo ni muhimu kwa mafundisho haya, ambavyo vyaweza kusaidia watu kuwa na ufahamu zaidi na msukumo wa kutekeleza waliyoyasoma. Katika **Sehemu ya Ziada A**. Iliyo katika ukurasa wa mwisho wa mwongozo huu kuna vifungu vya bibilia anbavyo vinahusika na sehemu tofauti za mafundisho haya.

### Utumizi wa talanta na vipawa

Katika hadithi ya bibilia kuhusu talanta, mwajiri alikasirishwa sana na mfanyakazi ambaye aliizika talanta aliyokuwa amepewa, lakini alipendezwa sana na wafanyakazi wengine waliotumia talanta zao kwa busara. Hadithi hii inatuonyesha ya kwamba sote tumetunukiwa "Talanta" – Ujuzi na uwezo. Tunapaswa kuzitumia. Katika hadithi hii, mtu ambaye alikuwa na talanta nyingi alihitajika kuzitumia vyema, vile vile, Yule aliyekuwa ametunukiwa chache, alitarajiwa kujiendeleza mbele na alichokuwa amepewa.

## Je, Ni nani atakaye tumia mwongozo huu?

*"Watu hupotea kwa kukosa ufahamu"*

Aliyenufaika na mafunzo haya

Mwongozo huu umeandaliwa ili kusaidia watu watakaotoa mafunzo haya. Mara nyingi, hawa ni watu walio na uzoefu mkubwa kama walimu au wawezeshi, hasa wafanyakazi katika miradi au mipango ya kupambana na ugonjwa wa Ukimwi.

Mambo muhimu ya kuzingatia katika mafundisho haya ni kuhimiza watu wanaoishi katika mazingira magumu (Mara nyingi, hawa ni watu waliolengwa kunufaika na miradi ya kushughulikia wanaoishi na virusi vya Ukimwi) katika jamii. Watu watakao nufaika katika kupokea mafundisho haya ni k.v; makundi ya kujitegemea, walengwa wa mradi, viongozi wa kijamii, washirika wa kanisa au wahudumu wa kujitolea wa wagonjwa nyumbani.

Wakati unapojaribu kutambua wahusika watakaonufaika na usaidizi wa kuanzisha riziki mpya, omba usaidizi kutoka kwa wenyeji walioko karibu. K.m. wakati wa mkutano wa baraza, unaweza kutoa changamoto hii kwa waliohudhuria; "Nyinyi mwajuana vizuri sana, na pia mnawajua watu miongoni mwenu wanaopata msaada kutoka kwa mashirika mengine. Je, mnaweza kuchagua watu walio dhaifu sana walio hapa?" Jamii au washirika wa kanisa huenda wakajua kwa mfano ni nani aliye na godoro, mbuzi moja au wawili, ni nani aliye angalau na kipande kidogo cha ardhi. N.k.

Inashauriwa ya kwamba, badala ya kuchagua mtu mmoja tu kutoka kanisani, shirika, au kikundi cha kijamii kupokea mafunzo, ili kuongeza ufanisi ni vema kuchagua watu watatu au wane kutoka pale ili kupokea mafunzo pamoja. Hii itawawezesha kusaidiana katika kutumia na kutekeleza mafunzo haya kwa ufanisi katika makundi au mashirika yao.

## Mbinu ya mafunzo

Ni muhimu kuzingatia kwamba mwongozo huu umeandaliwa kwa manufaa ya washirika wa makanisa, mashirika na makundi ya jamii ambao watapitia utaratibu huu kwa pamoja. Baadhi ya mazoezi husishi huwa na dhana kwamba wahusika wametoka jamii moja ama sehemu moja. Katika kipindi cha mafundisho, itabidi Mwezeshaji kurekebisha mazoezi husishi, iwapo wahusika wanatoka sehemu tofauti. K.m:

- Unaweza kugawanya wahusika katika vikundi vidogo kulingana na sehemu walizotoka.
- Unaweza kuchagua hali au jamii fulani ukizingatia na kutumia kama mfano.

Inashauriwa kwamba wahusika wote, licha ya uzoefu wao, kutumia mazoezi haya wakati wa mafundisho.

Taarifa muhimu hukusanywa na kuhifadhiwa katika kipindi cha mafundisho kwa kila somo/kipengele (**Sehemu 1–6**) ambazo ni nguzo muhimu za mafundisho haya. Taarifa hizi huletwa pamoja wakati wa kujibu "Maswali ya mwongozo" Taarifa hizi huchangia sana utaratibu wa kufanya maamuzi ya mwisho katika **Sehemu ya 7** – kusaidia wahusika na walengwa kutengeneza mipango na kuchukua hatua za kuboresha riziki yao



*Kundi la kujitegemea karibu na Lira, Uganda. (Picha: Jimmy Francis Odongo / Samaritan's Purse)*

### Makundi ya kujitegemea

Kujiunga na kikundi cha Kujitegemea (SHG) kunaweza kuwa njia bora ya watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (PLHIV) kupata usaidizi wa kukabiliana na matatizo yanayowakumba. Kujiunga na makundi kama haya, kunamaanisha kuwa na uwezo wa kufikia rasilimali. Pia inaweza kuwa ikawa njia mwafaka ya watu binafsi au familia kushawishi sera za mitaa, kwani watakuwa na sauti ya pamoja kama kundi.

Kuhimiza uundaji wa makundi ya Kujitegemea, (Mara nyingi hujulikana kama makundi ya akiba na mikopo) huenda kukawa ni utaratibu wa msaada sana kabla ya kuanza kutumia mwongozo huu. Makundi kama haya hutoa kundi lililo na msukumo wa kupenda utaratibu wa mafundisho ya lenzi ya riziki.

## Kusaidia mafukara (Maskini)

Ni jambo la muhimu sana kukagua wahusika watakao lengwa kwa mafundisho haya ili kuweza kutambua mitazamo yao kuhusu kutegemea misaada kabla ya kuwaalika katika mafundisho. Wakati mwingine, wanaotoa mafunzo wanatambulika vizuri kwa wanafunzi. Iwapo wahusika hawajulikani vyema kwa walimu, kufanya zoezi la kutambua vyeo vya ustawi Well being ranking) katika ukurasa wa ishirini na nne litasaidia kuwatambua walengwa halisi.

*"mafundisho haya yametufumbua macho;tumekuwa tukifikiri tuko chinina hatungeweza kufanya mambo mengi"*

Katika mazingira ambayo mashirika yamekua yakitoa misaada kila mara, wahusika huenda wakaweza kujikimu na kujitegemea wenyewe. Ni muhimu sana kusisitizia wahusika kuwa huu si mradi wa kutoa msaada bali nimchakato utakaowawezesha kuelewa zaidi yale waliyonayo na jinsi wanavyoweza kuendelea mbele. Baadaye katika mafundisho haya, huenda kukawa na msaada kidogo Kutoka nje mara tu wahusika watakapoweza kutambua na kutumia rasilimali zao katika kujiletea maendeleo endelevu. lakini hii haitafanyika kila mara.

*"Tulikuwa tukijiona hohehahe lakini sasa tunaweza kuanza bila fedha."*

Walionufaika mafundisho haya ya Lenzi nchini Kenya

Kwa hiyo, ni muhimu sana kwamba watu wanaohusika katika mafundisho haya waweze kujitoa na kuwa na msukumo binafsi wa kusonga mbele, kwani bila kufanya hivyo, wahusika huenda wakakata tama. Mahala watu wakotayari kwa mabadiliko, anza kwa kuwahimiza na kuwapa uwezo wa jinsi ya kutambua na, kutumia rasilimali walizonazo, hata kama wengine huenda wakawa na chache sana.

## Uzoefu unaowapatia uwezo

Kufuatilia mchakato huu ni zoezi linalo himiza na kuwapa uwezo, hususan walengwa ambao hawana matumaini ya siku za baadaye. Watu wasiojiweza wanasaidiwa kugundua uwezo mkubwa anbao Mungu amewapatia. Mafundisho haya yana andaa hata walio kwenye mazingira magumu sana kutazama maisha yao na rasilimali zao na kubaini fursa zilizopo ili kukabiliana na changamoto wanazo kumbana nazo.

Mafundisho haya yatawasaidia kuhisi wana dhamana na kuwasaidia kubaini ufumbuzi wa matatizo wanayokumbana nayo. Matokeo ya mwongozo huu yatakuwa ya msaada kwa watu binafsi, familia au makundi.

Mbinu hii ya lenzi haitoi kiwango cha ufumbuzi. Kila hali ni ya kipekee na inahitaji tafakari ya karibu ambayo lazima ifanywe kwa pamoja na watu watakaofaidika na hatua za kuingilia kati – kama hatua hizi zinahusu shughuli za vipato, utetezi wa haki za urithi za yatima na wajane au mikopo midogo midogo.

*"Lenzi ya riziki lazima iwe kama kinyonga: lazima ibadilishe rangi kulingana na mazingira. Lazima iwe tofauti katika kila sehemu."*

Mwezeshaji wa mwongozo huu

SOMO LA KWANZA

# 1 Maelezo ya jumla kuhusu mfumo wa riziki/maisha

Sehemu hii imeundwa kutambulisha mwongozo huu kwa makanisa, viongozi wa mitaa, mashirika na jamii mbali mbali. Itasaidia watu kuanza kuelewa utaratibu na manufaa Yaliyomo. Kufuatia mtazamo huu wa jumla, watu watakaonufaika na utekelezaji wa mafunzo haya watachaguliwa. Mtazamo huu pia utatoa utangulizi kwa wanafunzi waliochaguliwa.

Karibisha watu muhimu katika mkutano mahala panapofaa. Tambulisha mwongozo huu kama njia ya kusaidia watu kuwa na ufahamu zaidi kuhusu hali zao na mambo mengine ambayo yaweza kubadili riziki/maisha na kisha kuitikia kwa njia bunifu, hasa zile ambazo zitasaidia makundi dhaifu/yalio katika mazingira magumu. Wafahamishe kuwa mkutano hautachukua zaidi ya masaa mawili.

Anza kwa kuwaelekeza katika hadithi ya mtu ambaye amenufaika na mafundisho haya. Ni vyema kutumia hadithi unayoifahamu vizuri au tumia hadithi hii kutoka Nairobi, nchini Kenya:

### Kufikia uwezo wetu wa kweli

Kwa mara nyingi jamii, husahau thamani ambayo Mungu amewapatia watu wasiojiweza au wale wagonjwa. Mchango ambao watu hawa wanaweza toa kwa jamii hupuuzwa. Katika Kitabu cha bibilia, tunakumbushwa ya kwamba sote tumeumbwa kwa mfano wa Mungu – walio ambukizwa ugonjwa wa Ukimwi au wale ambao bado hawajaambukizwa. Sote tuliumbwa kwa sababu fulani, na kitu cha dhamana tunachoweza kutoa. Sisi sote. Mungu habagui. Binadamu wanaweza kuwa na ubaguzi Lakini Mungu hawezi!

Watu wanaoishi na Ukimwi wanamengi ya kuchangia katika jamii lakini, kama ilivyo kwa watu wote, wao pia wanahitaji mpenyo. Tafakari jinsi tunavyoweza kuwatiamoyo walioambukizwa kutumia vipawa vyao, au hata mali yao, ambayo Mungu amewatunukia.

Ni mambo gani katika jamii yetu au mila na tamaduni huleta ugumu kwa watu walioambukizwa na Ukimwi kuishi maisha yao kikamilifu? Tunaweza kufanya nini ili kuboresha hali hii?

## Kisa cha Mueni

Mueni ana umri wa miaka arobaini na moja na anaishi na virusi vya Ukimwi. Amejawa na furaha na heri njema, usoni mwake amejaa tabasamu. Amekuwa akifanya biashara ndogondogo kando kando mwa barabara katika kitongoji cha Kariobangi. Alianza kwa kununua na kuuza mboga na bidhaa zingine za shamba mpaka alipoamua kuuza leso na vitenge, biashara yake ilianza kudidimia na kisha ikafilisika.

Washirika wa kanisa liliko karibu naye walimwalika katika kikundi chao cha kusaidiana. Alikuwa mmoja wa wanafunzi waliopitia mafundisho ya mwongozo huu kanisani, baada ya mafundisho, alianza kuona sababu ya kuishi. Aliamua kurudi katika biashara ya ususi wa nywele alipogundua alikuawa na kipawa hicho ambacho hakukitumia hapo awali. Aliweza kukodisha kibanda na kuimarisha biashara yake ya ususi na kuongeza bidhaa zingine kama vile, nguo, nywele, n.k. Aliweza kujiunga na kundi la kuweka na kukopa. Yeye huweka akiba kutokana na faida anayopata kutoka kwenye biashara yake."Jambo la muhimu nililojifunza ni kuwa napaswa kuwa na fanya jambo – kama vile watu wenye ukoma kwenye mafundisho ya bibilia walivyoamua licha ya kupitia hali ngumu ya Unyanyapaa, kutengwa na hata kuchanganyikiwa (Luka 17:11-13)" Katika siku za usoni, Mueni anatarajia kununua vifaa vya kutengeneza na kusuka nywele na rasilimali zingine katika biashara yake. Sasa hivi, yeye ni kiongozi wa kundi hilo, jambo ambalo linathibitisha imani ya wenzake walio nayo kwake. Wanakusudia kuanzisha biashara ya kikundi kwa pamoja. Mambo haya yamemtia moyo sana na kumpatia ujasiri. "Nimejifunza kula tano na kuweka tano. Haya ni mafundisho ya ajabu na yenye kubadilisha sana" anasema kwa bashasha



*Mueni na mteja wake . (Picha: Moses Kamau Wanjiru / Samaritan's Purse)*

Elezea kwamba mwongozo huu unazingatia sana kuwawasaida watu dhaifu/walio katika mazingira magumu ili kuwawezesha kutumia vyema ujuzi na rasilimali walizonazo, na kuwawezesha kuwa na ufahamu bora wa mazingira yao ya mtaa. Mwongozo huu utajenga na kuwezesha nyumba, makundi na jamii kwa jumla kuongoza na kuamua utaratibu wao wa kimaendeleo. Mwongozo huu umetolewa kutoka kwa Muundo wa riziki/maisha endelevu, unaotumiwa na mashirika mengi.

Ushahidi muhimu wa matumizi ya mfumo huu wa maendeleo endelevu umetolewa katika sehemu ya mambo ya ziada (**Ziada B** katika ukurasa wa sabini).

*"Unaweza ukamsaidia mtu kwa kumpa lifti (kumbeba) kwenye gari lako ikiwa tu utamkuta barabaranii, na wala sio kama mtu huyo atakuwa nyumbani mwake, kwakuwa huwezi jua kama anania ya kusafiri."*

Mithali ya Kidholuo

ZOEZI

## Sehemu tofauti za mwongozo wa riziki/maisha


Embe ni tunda la kawaida ambalo huwa lenye utamu mwingi sana. Katika mwongozo huu tutatumia mfano wa embe ili kuelezea sehemu tofauti zilizomo ndani yake. Hebu tuchore embe kwa pamoja katika karatasi nyeupe.

Uliza watu wataje sehemu tofauti za embe kisha uchore picha kubwa ya embe hilo.

Kwanza tutaanza na sehemu ya juu ya embe ambayo, ndo **sura** yake, sura ya embe ndiyo huleta ushawishi wa kulifikiria au kulitamani, je , limeiva au ni tamu? Ni chachu au linawadudu? Sehemu ya juu ambayo bado ndo ngozi yake, inawakilisha hali au mazingira yetu. limeathiriwa na hali ya hewa, wadudu, magonjwa au lilijeruhiwa wakati wa mavuno? Vile vile, maisha yetu huathiriwa na masuala tofauti ambayo hatuna uwezo wa kuyabadili, ambayo hutufanya kuwa dhaifu/katika mazingira magumu

Kisha tunafikia sehemu ya ndani ya embe, sehemu iliyo tamu na yenye ladha. Lakini, hebu tazama embe linanini zingine ndani? **Nyuzi**! Maembe huwa na nyuzi nyuzi. Nyuzi hizi hushikilia embe na kudhibiti mtiririko wa maji matamu na hata kumtatiza anayelila. Nyuzi hizi huwa zimejisokota maishani mwetu hata kama hatuzioni sawa sawa. Zinawakilisha Sera, taasisi na utaratibu ambao huathiri maisha yetu vizuri au vibaya.

Ndani ya embe mna **Mbegu**, ambayo imejaa uwezo mkubwa. Mbegu inawakilisha rasilimali zetu, ujuzi wetu, marafiki ama familia. Rasilimali zozote ambazo familia iko nazo, hata kama ni chache mno, zinauwezo mkubwa sana iwapo zitatumiwa vizuri. Mbegu yaweza ikamea kuwa mti mkubwa wa mwembe unaozaa maembe mengi sana.



Kila sehemu ya embe huadhiri ile nyingine. Ngozi ya embe huenda ikajeruhiwa, mbegu huenda ikaoza ama likaiva sana. Hii ndiyo sababu kubwa ya kuzingatia kila sehemu.

Wakati tumelipata embe mkononi, lazima tuamue tunataka kulifanyia nini. Tunaweza tukaliuza, tukala lote zima au tukalipika. Maamuzi tutakayofanya ili kunufaika na embe hili kutokana na utamu wake au virutubisho vyake s. yanawakilisha "Mikakati" tunayoichagua na kuamua "Matokeo" yake

Embe linatupatia picha muhimu ya jinsi vipengele tofauti vya mbinu ya mwongozo huu zinavyoingiliana vizuri kwa pamoja. Mafundisho ya mwongozo huu yataangalia sehemu zifuatazo kwa kina katika:

- Rasilimali
- Udhaifu /mazingira magumu na jinsi ya kukabiliana nayo
- Sera, Taasisi,na Utaratibu wa mambo
- Mnyororo wa thamani
- Mikakati ya riziki/maisha
- Matokeo ya riziki/maisha



*Riziki kwa mara nyingi hufaidika na msaada kutoka kwa familia(Picha: Debora Randall / Samaritan's Purse)*

## Kutumia mbinu hii ya kutazama riziki/maisha

Kutumia mwongozo huu kutawasaidia wahusika kuelewa na kutumia uwezo (Rasilimali) na fursa wanazopata (mikakati ya riziki/maisha) zilizopo kwa ajili yao.

Mbinu ya mwongozo huu inaonyesha ya kwamba wakati watu wanafahamu njia za kufikia rasilimali tofauti na kuwa na uwezo wa kuzitumia, wataweza Kupunguza udhaifu wao/mazingira magumu. Hili ni jambo muhimu katika kumaliza umasikini.

### Kuna kanuni nne zinazo ongoza mwongozo wa mbinu hii ya riziki/maisha…

**KUZINGATIA WATU** Mwongozo huu unaanza kwa watu,watu walioathiriwa au wanaoishi na ugonjwa wa Ukimwi, watanufaika kabisa katika kutazama maisha yao, nguvu na uwezo wao.

**UJUMLA** Mwongozo huu unasaidia watu kuelewa uhusianouliopo baina ya mambo yote yanayo athiri maisha yao. Mambo haya huenda yako katika ngazi ya jamii au familia, au mtaani, kitaifa ama kimataifa.

**UWEZO WA KUBADILIKA** Maisha hubadilika kulingana na wakati.Mwongozo huu umenuiwa kuelewa na kujifunza Kutokana na mabadiliko, kusaidia mabadiliko mazuri na Kupunguza madhara ya mabadiliko mabaya. Mishtuko ya aina yote na mabadiliko ya pole pole kama vile mabadiliko hali ya hewa, magonjwa, majeraha au kuzorota kwa uchumi huenda kukaathiri riziki/maisha. Watu wanahitaji kufahamu athari za mashindano kutoka kwa wengine wanaotekeleza mikakati kama ile na kuchagua mikakati iliyo rahisi kubadilika.


**INAYODUMU/ENDELEVU** Riziki/maisha yapaswa kutoa matazamio ya muda mrefu. Inadumu au ni endelevu iwapo:

- Inastahimili shida na ugumu
- Haihitaji msaada wa nje (Isipokuwa kama msaada huu ni wa kudumu)
- Inatunza uwezo wa rasilimali asili kutoa mazao kwa muda mrefu
- Haidhoofishi au kuhatarisha riziki/maisha ya wengine.

ZOEZI

# Kuchunguza jinsi virusi vya Ukimwi huadhiri Riziki/maisha.


Zoezi hili linatazama jinsi Ukimwi huadhiri riziki/maisha. Bandikiza makaratasi manne kwenye ukuta au tumia ubao mweupe kuchora picha nne.



**PICHA YA KWANZA** Kwa uhusiano na kikundi, chora nyumba ya familia ya kawaida katika jamii pamoja na uwanja wake. Familia hii ina rasilimali nzuri (Kwa mfano, nyumba, mifugo, mimea katika shamba, maji, familia, watoto wanaosoma, kanisa linahusika. Nk.



**PICHA YA PILI** Eleza ya kwamba baba wa familia hii ameugua na hawezi kufanya kazi. Uliza madhara ya tukio hili katika familia? Kisha chora picha nyingine ukionyesha jinsi rasilimali tofauti zilivyoathirika kutokana na baba kuwa mgonjwa.



**PICHA YA TATU** Eleza zaidi kwamba baba amefariki dunia. (Chora kaburi) na mama pia ameugua. Pamoja katika kikundi, eleza katika mchoro jinsi familia ilivyoathirika. Je, mimea katika shamba, mifugo, nyumba, watoto, kuhusika kwa kanisa n.k. kumeathiriwa na kifo cha baba na maradhi ya mama.



**PICHA YA NNE** Sasa, chora mchoro ukionyesha kwamba mama amefariki dunia. Je, athari zake katika maisha ya watoto na uwezo wao wa kuishi ni zipi.

**Uliza wahusika maswali yafuatayo:**


- **Ni njia zipi ambapo maradhi ya Ukimwi yanaweza kuathiri riziki/maisha ya watu katika jamii?**
- **Ni riziki/maisha gani yanaweza kumfanya mtu awe dhaifu sana?**

Picha zilizo katika kurasa mbili zijazo zina Baadhi ya majibu.

### Uhusiano wa njia mbili uliopo kati ya ukimwi na riziki/maisha

Baada ya Kufupisha majibu ya wahusika,wezesha ubadilishanaji wa maoni haya. Hitimisha kwa kusisitiza uhusiano kati ya ugonjwa wa Ukimwi na riziki/maisha:

**Magonjwa na maafa (Yanayohusishwa na virusi vya ukimwi) yanaweza kudhoofisha mikakati ya riziki/maisha**




**Mikakati mingine yaweza kupelekea maambukizi ya Ukimwi**

Mtu anayeishi na virusi vya Ukimwi anaweza kuishi kwa miaka mingi sana kabla ya magonjwa sugu kujitokeza. Lakini muda huu wa afya njema huenda ukawa mfupi kwa watu wasio na usalama wa riziki. Hii ni kwa sababu ya lishe duni, kukosa kufikia matibabu bora, kukosa kupata msaada kutoka kwa marafiki, na mawazo sumbufu yanayo sababishwa na jitihada za maisha.

Wakati kuna usalama wa riziki/maisha, watu, familia, na jamii wanaweza kukabiliana vizuri na madhara tofauti yanayosababishwa na virusi vya Ukimwi.

## Jinsi ugonjwa wa Ukimwi unaavyoathiri riziki/maisha ya watu

| | |
|---|---|
| **Upungufu wa kazi** | Jinsi mtu anavyoendelea kuwa mgonjwa,kazi yao na ujuzi zinapungua katika nyumba yake. Wana familia ambao wana afya bora hulazimika kutumia wakati na uwezo walionao kumhudumia mgonjwa, na hili linawafanya kuwa na muda mchache wa kutafuta riziki. Wanaacha shule ili wafanye kazi hivyo basi kuathiri elimu yao. |
| **Kupoteza ujuzi na maarifa** | Iwapo wazazi watafariki mapema (kwa sababu ya magonjwa yanayotokana na Ukimwi), maisha na ujuzi wa kujitafutia riziki, hii ikiwa ni pamoja na maarifa ya ukulima hazipitishwi katika kizazi kipya. Hali hii huacha idadi ya kizazi kichanga bila uwezo wa kulima shamba au kusaidia familia zao. |
| **Kukosekana kwa Usalama wa chakula** | Kukosa kufanya kazi kila mara kunamaanisha ya kwamba kutakuwa na upungufu wa chakula mezani kwa kila mmoja katika familia. |
| **Kupoteza mali** | Wajane na mayatima wanaweza kuwa na shamba, nyumba na mali zingine ambazo wao hupokonywa baada ya kufariki kwa mme au baba |
| **Mabadiliko ya kijamii** | Familia zilizo na matatizo sugu ya kiafya hujikuta zinapata ushrikiano mdogo wa kijamii hasa pale watakapohitaji usaidizi wa kudumu kutokana na madhara ya ugonjwa wa Ukimwi. Unyanyapaa pia huenda ukasababisha familia hizi kutengwa. Miundo ya kijamii pia hubadilika na kujikuta kunaongezeko kubwa la kaya zinazoongozwa na wazee vikongwe au watoto. |
| **Udhaifu wa uwezo wa taasisi** | Elimu, afya, huduma za kilimo na kijamii zote huathiriwa kutokana na magonjwa na maafa yanayo husiana na Ukimwi. Ikiwa wafanyakazi hawapo kazini kwa sababu ya magonjwa, au kwa sababu ya kuwashughulikia wanaougua katika familia, ubora na wingi wa huduma zinazotolewa na taasisi hizi hupungua. Wafanyakazi waliosalia hulazimika kufanya kazi nyingi ili kuziba pengo lilioachwa na wenzao na hivyo kuongezea kazi yao na Kupunguza ubora wa kazi ile. |
| **Uharibifu wa mazingira** | Familia zilizoathiriwa na ugonjwa wa Ukimwi zinaweza kufikia rasilimali kama vile maji, shamba,au rasilimali za misitu, Lakini huenda wakashindwa kuzifikia na kuzitumia ipasavyo. Wakati umasikini unapoendelea kuzidi watu hupungukiwa na njia za mapato, kwa sababu ya Ukimwi, mazingira ya mtaa huenda yakatumika kupita kiasi na kuharibiwa kwa sababu ya mambo kama vile ukataji wa miti kwa sababu ya makaa au kuni au kulisha mifugo karibu na kijiji. |

# Jinsi riziki/maisha inaweza kuweka watu katika hatari ya kupata virusi vya ukimwi

| | |
|---|---|
| **Kuongezeka kwa hatari ya maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi** | Riziki/maisha yanayohusu kazi za kigeni, safari za usiku, huchangia kuongezeka kwa hatari ya kuambukizwa Ukimwi kwa wanaosafiri na wanaoachwa nyumbani. |
| **Umasikini** | Wake kwa waume huenda wakajikuta wamejingiza kwenye biashara ya ngono (kwa mfano, kufanya ngono kama malipo ya ufyekaji wa uwanja, ngono ili kupata chakula, Kufanya ngono na mwenye nyumba kama malipo ya kodi ya nyumba pale kodi imekosekana) pale mikakati mingine ya kupata riziki/maisha inapokuwa imeshindikana, na kujiweka kwenye hatari ya kupata maambukizi ya virusi vya Ukimwi. Wanawake na wasichana huenda wakalazimika kuingia katika mahusiano ya ngono isiyo salama |
| **Kupungua kwa kupata dawa za kupunguza makali ya Ukimwi (ART) na tiba ya kifua kikuu** | Upatikanaji wa dawa za kupunguza makali ya Virusi vya Ukimwi na Kifua kikuu ni muhimu sana kwa watu wanaoishi na VVU ili kuwezesha kuishi maisha marefu na yenye afya bora. Kwa bahati mbaya, si rahisi kwa watu wasio na riziki/maisha salama kufikia huduma hii. Gharama za usafiri kufika kwenye vituo vya matibabu na gharama za matibabu ni miongoni mwa matatizo yanayowakabili watu wanaoishi na VVU. Wakati mwingine hushindwa kuhudhuria kliniki/hospitali hasa kwa wale walioajiriwa na wale walio na watoto au wanaowahudumia wagonjwa majumbani. Zaidi ya hayo, watu wanaoishi na ugonjwa wa Ukimwi, hupatashida kufuatilia matibabu bila msaada na pia huenda wakaathirika kutokana na lishe duni. |

## Maswali ya Mwongozo

Ili kuhakikisha ufafanuzi kamili, maswali haya ya mwongozo yamewekwa pamoja katika kila somo. Lakini, sio lazima kuyajibu maswali yote kwa pamoja katika kila somo. Wawezeshaji wanaweza kufanya mafunzo haya kuwa rahisi kwa kuyabadilisha ipasavyo na kutia moyo wahusika kujibu maswali moja kwa moja, kufuatia vitendo.



*Uuzaji wa chakula ni mkakati bora wa riziki. (Picha: Moses Kamau Wanjiru / Samaritan's Purse)*

## 1 MASWALI YA MWONGOZO Maelezo ya jumla

Maswali haya huenda yakawasaidia wadau wote kufikia maamuzi ya mipango ya baadaye wakizingatia yale waliyoyasoma. Maswali haya yatakuwa ya msaada mkubwa iwapo yatajadiliwa katika makundi madogo.

Wakati unayatumia maswali haya pamoja na wanafunzi, jadili maswali mawili ya mwanzo tu.

**1a** **Je, kulingana na ufahamu wako, umeona manufaa gani katika mafundisho haya?**

**1b** **Kutokana na mafundisho haya, ni nini chaweza kubadilika?**

**1c** **Ni jinsi gani mafundisho haya yanaweza kunufaisha shughuli za kupambana na Ukimwi kwa maisha ya mnao walenga?**

**1d** **Je, ni vipi twaweza kusonga mbele na mipango ya mafundisho haya?**

**1e** **Ni nani angefaa zaidi kupokea mafundisho haya?**

# Kufikia makubaliano/ Hitimisho

Kwa pamoja, kubalianeni tarehe za mafunzo ya mwongozo huu na mahala yatakapofanyikia.

Wadau wote wanapaswa kujadiliana mbinu ya kuwachagua wanaotarajiwa kuwa wahusika: ufahamu wao mbinu hii (Si Mbinu ya msaada), kujitolea kwao katika kuhudhuria mafundisho yote, nia ya kutaka mabadiliko, ngazi tofauti za udhaifu/mazingira magumu, na pia kuhakikisha usawa wa kijinsia. Kila somo lapaswa kuwa na angalau wahusika kati ya ishirini na arobaine

Kama unapania kuiga mafundisho haya, basi chagua watu watatu au wane kutoka kwa jamii moja au kanisa au shirika ambao wana uzoefu wa kufundisha na ambao wanataka kuwa wataalamu katika kutekeleza mfumo wa mwongozo huu.

Unaweza kuwafundisha moja kwa moja, peke yao au pamoja na walengwa. Mfumo wa mwongozo huu si rahisi kutekeleza kwa hivyo ni muhimu kuhakikisha kwamba wanaweza kuwafundisha wengine ipasavyo.

Utahitajika kutoa msaada wa kudumu katika kushauri na kuwawezesha jambo ambalo litachukua muda mrefu, Watahitaji msaada wakati watayarudia mafundisho. Ukiwachagua watu watatu au wane kutoka kwa jamii moja, kanisa au shirika, watasaidiana katika kubadilishana mafunzo na wengine.

### Sisi sote tuna uwezo

Wakati mwingine sisi hupuuza uwezo wa watu hasa wale wanaodharauriwa: walio dhaifu/katika mazingira magumu, maskini, walio na Ukimwi, n.k. Lakini mbele za Mungu sote tuna uwezo. Hebu nyosha mkono wako. Tazama vidole vyako kikiwemo kidole gumba. Ni kipi kilicho na nguvu? Ni kipi kilicho kikubwa? Ni kipi kinachoonekana kinyonge sana? Ni kipi kinategemea kingine ili kutenda kazi vyema?


Sasa, hebu kunja mkono wako kama ngumi – kama unataka kuchukua kitu fulani ili kuchukua hatua fulani. Tazama vidole vyako katika msimamo huu. Haijalishi mtazamo wako kuhusu kilicho na nguvu, kilicho kikubwa, ama kilicho kinyonge sana, katika msimamo huu, (Msimamo wa hatua na nguvu) vyote vinafanana. Kila kidole hufanya kazi yake, pamoja na jirani yake. Huu ni mfano mwepesi wa thamani sana kama watu wa Mungu.

## Kisa cha Mwangi.

Mwangi anaishi na Ukimwi, katika nyumba yake na mkewe na watoto wane katika kitongoji duni cha grogan nchini Kenya. Yeye na familia yake wanashukuru sana kwa kupokea mafundisho haya ya Riziki/ maisha kutoka kwa kanisa lao. Wakati Mwangi alipatana na Kanisa mara ya kwanza, alikuwa mgonjwa na amelazwa kitandani bila matumaini na amekata tamaa. Kanisa lilianza kumpa huduma za kiroho na zile za kimwili mpaka wakati alipopata nafuu, na akaanza kujishughulisha kwa kufanya biashara ndogo kwa mtaji wa shilingi mia sita alizopewa na kanisa. Alianza kwa kununua maziwa ya kuuza, ingawaje kwa mara nyingi alikuwa mgonjwa na hili liliathiri biashara yake.Baada ya kupokea mafundisho haya, aliamua kubadili biashara ya maziwa na kuanza biashara ya kuuza nguo za mtumba. Yeye huzinunua mjini Nairobi, anaziosha, anazirekebisha, anazipiga pasi ambayo, hutia thamani kidogo na kisha kuzipeleka vijijini ambako ameweka mpango mzuri sana wa kuuza kupitia vijana wa mitaani.Yeye hununua nguo zile kwa kiasi cha shilingi ishirini kila moja na kuziuza kwa takribani shilingi mia sita. Sasa wanashirikiana na mkewe na wameweza kununua vyereani viwili. Kutokana na mafunzo haya, wameweza kuanzisha kikundi cha kuweka na kukopa ambapo Mwangi ndiye mwenyekiti. Yeye huwahimiza wenawake katika kikundi chao ambao ni wagonjwa na hutumia mfano wake wa kupambana na changamoto za maisha na kuwapa mbinu za kujitegemea ili kukabiliana ugumu wa maisha. Sasa hivi, Mwangi ameweza kulipa mahari kwa familia ya mke wake na huisadia jamii yake vizuri kulipia gharama za kupangisha nyumba,mavazi na chakula. Ni mtu anaekopesheka na mwenye uwezo wa kukopa mpaka kiwango cha hadi shilingi elfu thelathini na hata kuwasaidia wengine. “Nilikuwa nimedharauliwa na kutengwa na watu wa ukoo wangu na hata marafiki, Lakini sasa, mimi ni nuru kwa maisha yao. Nashukuru kwa mafunzo haya, nimeweza kuona fursa ambazo hapo awali sikuweza kuziona. Asante”.

SOMO LA PILI

# 2 Utambuzi wa rasilimali




Rasilimali ni nguzo muhimu ambayo familia zaweza kutumia kujenga mikakati yao ya riziki/maisha. Uwezo wa watu kuepukana na umasikini unategemea sana rasilimali wanazoweza kufikia.

Watu hutumia rasilimali zao kukabiliana na migogoro ya maisha. (Kama vile, Mishtuko, mizunguko na mienendo) wakati watu wanapofikiria kuhusu rasilimali, wao hufikiria tu kuhusu fedha na mali kama nyumba – rasilimali ambazo watu maskini sana hawawezi kufikia. Hata hivyo, kuna aina sita za rasilimali na wakati watu wameanza kufikiria kuhusu ujuzi, marafiki na wana familia, wanaanza kuona kwamba wana rasilimali.

## Mifano ya rasilimali

| | |
|---|---|
| **Binadamu na kiroho** | Hizi ni mali ambazo mtu binafsi anazo. Kama vile, elimu, imani, afya bora na, nguvu za kimwili, uzoefu wa maisha na hekima, akili na ujuzi, rasilimali za kiroho ni kama vile maombi, ushirika na Tumaini. |
| **Rasilimali ya kijamii** | Hii ni rasilimali inayohusu mitandao ya usaidizi – familia na marafiki, watu wa ukoo, makundi ya kidini, au mashirika mengine ambayo wao ni wanachama. Kwa mfano, makundi ya kilimo, makundi ya kuweka na kukopa na makundi ya kusaidiana ya wanaougua Ukimwi. |
| **Rasilimali ya kisiasa** | Hii ni rasilimali inayo onyesha nguvu ya watu katika jamii na familia. Inahusu uwezo wa watu kushawishi maamuzi, kufanya utetezi wa ugawaji wa mali au mabadiliko, na uwezo wa kudai haki (Kama vile Shamba, elimu, matibabu au kupiga kura). |
| **Rasilimali ya kiumbo** | Rasilimali ya kiumbo, pia inajulikana kama mali inayoonekana, ni kitu ambacho kina thamani. Rasilimali hii ni dhahiri. Ni mambo ambayo ni muhimu aidha yenyewe, au inayozalisha thamani kwa mmiliki. Kwa mfano, rasilimali hii ni kama vile,nyumba, vifaa na zana, baskeli, gari, visima, mavazi na kadhalika. |
| **Rasilimali ya kifedha** | Hii ni mali kama vile fedha taslimu, au mali nyingine ambayo yaweza ikabadilishwa kuwa pesa taslimu kwa haraka na wepesi. Pia huenda ikahusu nafaka,mifugo,dhahabu,mshahara,fedha kutoka ng'ambo na kadhalika |
| **Rasilimali asili** | Hii ni mali kama vile ardhi, maji, mimea, mifugo, hewa, mvua ya kawaida na bahari au ziwa. Mali asili haiwezi ikadumu kama kuna ufugaji wa kiholela, ukataji wa miti kwa sababu ya makaa, au kuni, utumizi mbaya wa ardhi. Haya ni mambo ambayo watu walio na nafasi chache za mapato hawawezi kuepuka. |


Watu wengine huweka rasilimali ya kijamii na Kisiasa kwa pamoja au kutenganisha mali ya kiroho na kimaumbile. Haijalishi jinsi utakavyoziunganisha kwa pamoja cha muhimu hapa ni kuona rasilimali hizi zote zimehusika.

ZOEZI


# Athari za Virusi Vya Ukimwi katika upatikanaji wa mali

Tunahitaji kufikiria zaidi ya mambo ya kawaida ili kuvumbua rasilimali zote wanazoweza kufikia. Kunaweza kuwa na rasilimali zilizojificha ama uwezo mwingine ambao watu hawajawahi kufikiria kutumia katika njia ya ubunifu. Hapa kuna zoezi rahisi la kusaidia katika kufikiria nje ya Kisanduku. (Kidokezo: Usiwaambie wahusika jina la zoezi hili – waambie tu ni njia ya kutafuta majibu bunifu ya matatizo.

Chora mraba huu kwenye chati ama ubao mweupe. Ruhusu kama dakika kumi tu ili kuwezesha wahusika kuunganisha vinukta ukitumia mistari minne bila kuinua kalamu kutoka kwenye karatasi. Tazama majibu ya wahusika. Kuna mhusika anayeweza kulipata jibu ingawa watu wengi watatofautiana kutafuta suluhisho katika pembe nne za Kisanduku/mraba. Iwapo hamna mtu yeyote aliyepata jibu la kweli, onyesha jinsi vinukta hivi vinaweza kuunganishwa kwa mistari iliyochomoza nje ya Kisanduku.



*Je unaweza kuunganisha vinukta hivi vyote ukitumia mistari minne pekee bila ya kuinua kalamu kutoka kwa karatasi?*



*Jibu litahitaji kufikiria nje ya Kisanduku.*

## Madhara ya Ukimwi katika kufikia rasilimali

Familia zilizoathiriwa na Ugonjwa wa Ukimwi mara nyingi hujikuta hazina uwezo wa kufikia rasilimali kikamilifu. Kwa mfano Maarifa na ujuzi unaweza kupotea wakati wazazi wameaga dunia kabla ya kuwafundisha watoto wao. Unyanyapaa na kutengwa kunaweza kupunguza rasilimali ya kijamii, iwapo familia zimeondolewa kanisani, shuleni, ama kwenye makundi mengine katika jamii. Mila za urithi wa mashamba zinaweza kupelekea Wajane na watoto yatima kuwa dhaifu na kuishi katika mazingira ngumu katika tamaduni zajamii nyingi

Familia hizi hulazimika kuuza mali zao muhimu (Kama vile baskeli, mifugo, zana za kilimo n.k.) iwapo wanafamilia wanaougua jambo ambalo huathiri uwezo wao wa kupata mapato siku za baadaye. Kuongezeka kwa gharama za matibabu na gharama za mazishi hua mzigo mkubwa sana kwa jamii zilizoathiriwa.

Kwa familia ambazo ni dhaifu sana, rasilimali yao kubwa sana ni uhusiano walio nao na wengine na uwezo wao wa kuomba msaada kutoka kwa mitandao hii ya kijamii. Hii ni pamoja na familia kubwa, marafiki, kanisa, wachungaji, washirika wa kanisa, uhusiano na makundi yaliojipanga na mashirika ya kimaendeleo.

*"Matumaini ndiyo yamenipa ari ya kuishiNaamini kwamba nitaweza kufanya mambo makubwa sana maishani."*

Aliyenufaika kwa masomo haya.

ZOEZI

# Kutambua Rasilimali


Toa michoro ya mifano ya rasilimali katika **Sehemu ya Ziada C** katika kurasa 71–79 kisha uikate.

Waulize wahusika kujadili rasilimali nyingi iwezekanavyo kwa muda wa dakika tano hivi. Kisha uyaandike matokeo ubaoni.

Baadhi ya rasilimali zitakazotajwa sana ni zile za kiumbo na kijamii. Hoji zaidi ili kupata mifano mingi ya rasilimali za kibinadamu, kisiasa, Kiroho na Kifedha. Toa zile picha kisha uwaulize wazilinganishe na zilizo kwenye picha.

Sasa waulize watatue na waziweke kwa aina zinazofaa.(uliza mhusika mmoja kuchora kwa ubao rasilimali zilizosahaulika)

Iwapo watu wanapata shida kufikiria kuhusu rasilimali, wawezeshe kufikiria kuhusu mifano ya riziki na aina ya vifaa, zana au mali inayohitajika ili kutekeleza ujuzi fulani. watazamishe jinsi rasilimali tofauti zinavyoweza kutumika kwa pamoja kama msingi wa riziki/maisha. Kwa mfano, uliza ni rasilimali gani zinahitajika katika kilimo (Majibu huenda yakahusu Ujuzi, uzoefu, maarifa, shamba, plau na fahali wake.






## Makao mapya, Tumaini jipya

Gomose ni mjane mkristo aliye na watoto wanaoishi kusini mwa nchi ya Uhabeshi. Nyumba yake ya mabanda ilihitaji marekebisho Kila mara alikuwa na wasiwasi mkubwa kwamba nyumba yake huenda ikabomoka. Kipindi cha msimu wa mvua, nyumba yake ilivuja, na kuharibu bidhaa zilizoko humo ndani. Nyumba yakehaikumlinda kutokana na upepo mkali. Kanisa la Kale Heywet lilitoa mafundisho ya riziki/maisha kwa watu thelathini na wawili, akiwemo Gomose. Wawezeshaji kutoka kanisa hili walifanya matembezi ya nyumbani kwa wahusika wote waliolengwa kwa mafundisho haya. Kwa pamoja, walitathmini uwezo wake na mali aliyokuwa nao. Alikuwa na mti mkubwa wa aina ya mkaratusi (Eucalyptus) katika uwanja wake . kundi la kanisa likapendekeza kuukata mti ule ili kupata mbao za kujenga nyumba na kutatua tatizo lake la makazi.Watu wengi mno walikuja kumsaidia Gomose – majirani, watu wa ukoo, washirika kutoka kanisani na vijana. Walikuwemo maseremala walioiunda nyumba ile. Majirani walileta misumari, vifaa na kujitolea katika ujenzi wa jengo hilo. Kikundi cha uimbaji kutoka kanisani pamoja na kundi la vijana walichimba msingi wa nyumba ile. Kanisa pamoja na maafisa wa serikali walitoa mchango wao wa mabati na kwa pamoja, jitihada hizi zilifanikisha ujenzi wa nyumba mpya ya Gomose.Gomose hakuwa na hatimiliki za nyumba au kipande cha ardhi ile. Kanisa liliingilia kati kumwezesha kupata hati za umiliki ili kuwa na ulinzi wa siku za usoni. Ujenzi wa nyumba yake ulipokamilika, mikakati ya riziki/maisha ilichunguzwa kwa makini. Baadaye, alinufaika na mafunzo ya kilimo cha bustani ya mbogamboga na mimea mingine karibu na nyumba yake. Mavuno humwezesha kulisha familia yake na mauzo ambayo humletea mapato. Hivi sasa, ana furaha nyingi mno ambayo kulingana naye, imetokana na mafundisho ya mwongozo huu.



*Shamba la gomose (Amekuza kabeji na mandizi-vyakula vinavyoweza kustahimiliukame (Picha: Tamene Tessema / Tearfund)*

### Baadhi ya rasilimali zilizotumika kumsaidia Gomose

| | |
|---|---|
| **Binadamu na Kiroho** | Kanisa, ajira, hekima na imani |
| **Rasilimali ya Kijamii** | Marafiki, familia, ushirika wa Kebele (ulitoa mabati, milango na dirisha) watu walishirikiana |
| **Rasilimali ya Kisiasa** | Uwezo wake wa kudai haki ya shamba lake, utaratibu wa serikali na watu waliotambua utaratibu wa serikali na walihusika kumwelekeza |
| **Mali asili** | Miti |

## Kubaini/kuchunguza rasilimali

| | |
|---|---|
| **Rasilimali Za Kibinadamu na kiroho** | Je, familia ina maarifa au ujuzi wa aina gani ambao unaweza kuwasaidia katika riziki/maisha yao? Kwa mfano, kukausha matunda, kutumia mimea ya matibabu, kutengeneza sabuni au kupika sambusa. Je, wamefika kiwango kipi cha Masomo rasmi na yasiyorasmi? Je, wana familia wana afya bora na nguvu za kufanya kazi? Kama la, kwa nini? Je, ni kwa sababu ya magonjwa au lishe? Wamekumbwa na magonjwa ya aina gani kwa muda wa mwaka moja uliopita?Je, wao huamini Mungu? Imani yao iko hai? Wao huomba – peke yao au na watu wengine? Imani zao za kidini zinawapa matumaini? Wanaamini Mungu ana mipango mizuri kuwahusu? (Yeremia 29:11). Wao hupata motisha kutoka kwa kanisa au msikiti? |
| **Rasilimali za kijamii** | Wao hupokea msaada (Wa kifedha au vitendo) Kutoka nje ama kwa familia ya karibu, marafiki, majirani, ukoo ama kwingine? Je ni msaada wa aina gani na mara ngapi? Ni miundo ipi ya kijamii ipo? Wao wana uhusiano na makundi ya kilimo, akiba na mikopo? Makundi ya kusaidiana ama makundi mengine? |
| **Rasilimali za kisiasa** | Familia hizi zina mfumo upi wa kisiasa? Je, wao wana uhusiano upi na ama ushawishi na mtu yeyote aliyeko madarakani? Kwa mfano wao ni wana kamati? Wana uwezo wa kuwafikia viongozi au wanasiasa, mashirika yasiyo ya kiserikali au makanisa yaliyo na ushawishi mkubwa au wajumbe wa serikali? |
| **Rasilimali za kiumbo** | Familia inamiliki nini kinachoweza kuwasaidia kupata mali? Kama vile baskeli, mifugo, au vifaa. n.k? rasilimali hizi zinatumika vipi? Je, nyumba wanayoishi ni ya kupangisha au ni yao binafsi? Je, wanaweza kupata huduma zozote za maji na usafi wa mazingira? Je, wanapata huduma za usafiri? (gari ama basi n.k.)? Je, kuna barabara za kufika sokoni? |
| **Rasilimali za kifedha** | Je, wana akiba yoyote? Je, wanahifadhi akiba hii katika mifugo, pesa taslimu, vito vya thamani ama katika biashara? Je, familia hii hupata mikopo? Je wana mbinu gani za kujitafutia mapato? Je, wanatumiwa pesa kutoka ngambo? Je, wana pesa za kutosha za kulipia karo ya watoto? |
| **Rasilimali za asili** | Je, familia hii ina miliki ardhi? Iwapo hawamiliki shamba je hujishughulisha na shughuli zozote za shamba? Je, ni kiasi gani cha shamba wao hulima? Wao huitumia vipi? Je, shamba hili lina mazao mengi? Hupata mvua za kutosha? Je familia hizi huhifadhi maji ya mvua, kwa matumizi wakati wa ukame? Je wana uwezo gani wa kufikia rasilimali asilia kama vile maji, mimea, miti, mvua au Uvuvi wa samaki? Uliza kuhusu idadi, ubora na matumizi yake? Familia hii ina mifugo ya aina gani? Na mazao ya a gani ya shamba? |



*Fahali na plau ni rasilimali za kiumbo zilizo na thamani sana (Picha: Debora Randall / Samaritan's Purse)*

# 2 MASWALI YA MWONGOZO Rasilimali

Maswali yafuatayo yatawasaidia watu binafsi na makundi kutathmini hali yao kulingana na rasilimali na kuwawezesha kutambua suluhisho lao wenyewe. Hakikisha kwamba wahusika wameyaelewa maswali vizuri. Chukua muda mfupi kuwaelezea kuhusu maswali hayo ili wahusika wote katika kikundi wawe na utulivu na waweze kuhusika na kuchangia vizuri. Nakili majibu yote ya wahusika kwenye chati iliyo na **Maswali ya Mwongozo Sehemu ya 2**, katika ukurasa 21. Wakati unauliza maswali haya katika jumuia huenda ikawa si mwafaka kutumia chati hii. Nakili majibu haya kwingine kisha ujaze majibu kwenye chati baadaye. Unaweza ukaachia wana jumuia sehemu moja ya majibu na kisha nakala nyingine isalie na Mwezeshaji. Kwa kufanya hivi, utaweza kufuatilia maswali muhimu na kisha baadaye yatakuelekeza katika mwongozo huu.

**ZINGATIA:** Ni vyema zoezi hili kufanyika kwa pamoja katika kikundi; hata hivyo, ni halali pia likifanywa na mtu binafsi. Chati ile, ile yaweza kutumika.

Kwanza kabisa, pitia kila aina ya Rasilimali ukitumia ujumbe uliyo kwenye Kisanduku **Kutambua rasilimali** (Ukurasa 19) katika kutanguliza kila rasilimali. Kisha tazama kila rasilimali wahusika wanaweza kufikia. Maswali haya yatawezesha wahusika kufikiria kwa undani kabisa na "Nje ya Kisanduku" kuhusu ufikiaji wa rasilimali zao. Tumia kadi ndogo zilizoko katika **Sehemu ya Ziada C**. Kama vielelezo wakati wanajadiliana majibu ya maswali haya. Hili litawezesha wahusika kuzingatia uwezekano wa rasilimali zote.

**2a** **Tazama rasilimali zote ambazo familia zinaweza kuzifikia. Ni rasilimali gani za muhimu sana, zilizo imara (Strong) na zilizo na mazao sana ya kuhakikisha uhai na ustawi?**

Tumia maswali yaliyo katika Kisanduku **kutambua rasilimali** kusaidia watu kuzingatia majibu yao. Chagua (Ama chora) kadi inayostahili kila mara kama kielelezo

**2b** **Ni rasilimali zipi, familia zenu hufikia ambazo si imara lakini zina uwezo mkubwa lakini ni chache na hazitumiki ipasavyo kuboresha maisha yao?**

Mara nyingine, tumia ujumbe uliyo kwenye kisanduku na kadi ili kusaidia watu kufikiria kuhusu rasilimali.

**2c** **Ni rasilimali gani zingine zipo katika jamii lakini familia hazifikii vizuri wakati huu? Nani ndiye anazifikia (K.v. Maji, mali ya umma na huduma za umma ?**

Rasilimali hizi huenda zikawa zinamilikiwa na jumuia na pengine si kila mtu anaweza kuzifikia. Ni nini kinazuia familia katika kufikia rasilimali hizi? Mara nyingi kuna rasilimali zingine za kijamii hukaa bila ya kujulikana, Kama vile maji, vyoo, bustani ya jamii, shamba la umma, miti ya matunda, viongozi wa vijiji na huduma za umma. Hata maafisa wa kilimo wa serikali na mbegu za bure (ruzuku) au zilizopunguzwa bei na vifaa vilivyo katika jumuia hii, vinaweza vikatambuliwa kama rasilimali za jamii. Tumia kadi tena kutambua rasilimali za aina hii.

**2d** **Ni nini kinawazuia kufikia na kutumia rasilimali hizi zingine?**

Jadili rasilimali zilizotambuliwa katika maswali 2b na 2c. Baini ni nini kinazuia rasilimali hizi kutumika.

**2e** **Ni nini Tunaweza kufanya ili kuboresha matumizi ya rasilimali zilizopo na kuongeza uwezo wa rasilimali zingine?**

Tambua kitendo cha kuboresha matumizi ya rasilimali iliyotambuliwa hapo juu.

MASWALI YA MWONGOZO YA SEHEMU YA 2

# Rasilimali

| | **2a** Je, familia zenu huweza kufikia rasilimali zipi muhimu? | **2b** Ni rasilimali zipi, familia zenu hufikia ambazo zina uwezo mkubwa lakini ni chache na hazitumiki ipasavyo kuboresha maisha yao? | **2c** Ni rasilimali zipi zingine ambazo zipo katika jamii lakini familia zenu hazifikiwi vizuri wakati huu ? | **2d** Ni nini kinawazuia kufikia na kutumia rasilimali hizi zingine ? | **2e** Ni nini Tunaweza kufanya ili kuboresha matumizi ya rasilimali zilizopo na kuongezea uwezo wa kufikia rasilimali zingine zilizo katika jumuia ? |
|---|---|---|---|---|---|
| **Binadamu na kiroho** | | | | | |
| **Kijamii** | | | | | |
| **Kisiasa** | | | | | |
| **Kiumbo** | | | | | |
| **Kifedha** | | | | | |
| **Mali Asili** | | | | | |

SOMO LA TATU

# 3 Kuelewa mazingira magumu na jinsi ya kukabiliana nayo

Uwezo wa watu na jamii katika kukabiliana na majanga yasiotarajiwa na matukio magumu maishani una uhusiano wa karibu na mali waliyonayo. Uwezo wa watu kukabiliana na mambo mazito au mazingira magumu hutegemea kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa rasilimali na kama wanaweza kulinda na kudumisha rasilimali hii wakati wa shida au baadaye.

Mazingira magumu ni neno linaloelezea jinsi watu wanavyoweza kusimamia, kukabiliana na ama, kuishi wakati wa matukio magumu, migogoro au hatari. Kwa mfano, familia zinazoishi kwenye nyumba zilizojengwa vyema huenda wakaepuka madhara ya upepo mkali au Mawimbi ikilinganishwa na familia zinazoishi kwenye nyumba zilizojengwa vibaya.

Kuna aina tofauti za majanga au migogoro.

- Mishtuko (Shocks)
- Mizunguko (Cycles)
- Mienendo (Trends)

Tazama kwenye Kisanduku kifuatacho.

## Mishtuko, Mizunguko na Mienendo

**MISHTUKO (SHOCKS):** Haya ni matukio ya ghafla ambayo yanaweza kuumiza maisha ya watu na riziki zao. Mifano ya mishtuko ni kama vile, Vimbunga, mafuriko, vita vya wenyewe kwa wenyewe , kifo cha mmoja wa familia, kipindupindu au kupoteza kazi.

**MIZUNGUKO (CYCLES):** Hii ni mishtuko inayotokea mara kwa mara. Wakati mwingine unaweza ukayatarajia na kujiandaa vyema. Mifano yake ni kama vile mafuriko ya msimu, magonjwa yanayotokea wakati wa mvua, au bei ya mazao kushuka baada ya mavuno na kupanda juu wakati wa uhaba wa chakula.

**MIENENDO (TRENDS):** Haya ni mabadiliko mazuri au mabaya kwa muda mrefu. Ni vigumu kubaini kama mienendo mingine hutokea pole pole. Mfano ni kama vile, kuimarika au kudorora kwa uchumi wan chi, kupanda kwa bei ya mafuta, mmomonyoko wa udongo, misitu na mito,kubadilika kwa misimu ya mvua, au maambukizi ya Ukimwi katika nchi. Wakati unatathmini mienendo hii, ni vyema kujiuliza je imekuwa hivi kila mara? Mambo yanabadilika? Kama ndiyo, vipi?



ZOEZI

# Kuelewa ngazi za mazingira magumu

Katika mazingira ya migogoro, idadi nzima ya watu huenda wakawa katika hatari. K.m mafuriko (Maporomoko ya ardhi, vita au magonjwa kama vile ya Ukimwi), lakini udhaifu (Mazingira magumu) na ushujaa wa watu binafsi na familia kwa matokeo ya kushtua inatofautiana. Kwa kupata ufahamu mzuri wa udhaifu wetu, tunaweza kujiandaa vyema kujibu hali za kuhatarisha.

*"Hauwezi ukafahamu unapoelekea hadi ujue mahali unapotoka."*

Aliyenufaika kwa mafunzo haya

Tunapaswa kutazama kwa undani jamii yetu. Je, ni neno gani tutalitumia kuelezea ngazi tofauti za umasikini na udhaifu?

Chora picha kama ilivyo hapa chini kwenye ukurasa na uandike mada zake. Katika upande wa kushoto mwa picha, andika yale maneno mmekubaliana, baada ya majadiliano, kwa ngazi tofauti.

Jadili na kubali maana ya maneno haya. Katika picha ile hapo katikati, eleza zaidi kila neno.

Ni vigezo vipi vitatumika kutambua ngazi gani? mtu binafsi au famila zipo? Jadili zaidi vigezo hivi kasha uyaandike kwenye upande wa kulia.

### Mfano wa ngazi za umasikini na mazingira magumu.

| Matamshi ya kawaida | Maelezo | Vigezo |
|---|---|---|
| Sio katika mazingiara magumu | Wale ambao wanakabiliana vizuri | Wana nyumba yao nzuri ya kudumu,rasilimali kadhaa na mapato ya uhakika |
| Karibu na mazingira magumu | Wale wanaokabiliana sawa sawa lakni mshtuko unaweza ukawasukuma chini ya mstari wa umasikini | Walio na nyumba iliyo na paa nzuri na rasilimani kidogo.mapato sawa |
| MSTARI WA UMASIKINI | | |
| Katika mazingira magumu lakini uchumi uko hai | Wale ambao kwa kawaida wanaweza kukabiliana | Wana nyumba ndogo,iliyo na uwezo wa kudhibiti hali ya hewa, rasilimali kidogo. Mapato yasiyo ya kutegemewa na kwa kawaida hutokana na kazi za mkono ama uuzaji kwa vibanda |
| Katika mazingira magumu sana | Wale ambao wanaweza kukabiliana lakini kwa ugumu | Kwa kawaida wana nyumba ndogo ya udongo iliyo na paa inayovuja. Rasilimali chache mno na mapato yasiyo yakawaida |
| Fukara au maskini sana (Hohe hahe) | Wale ambao hawawezi kukabiliana | Hawana nyumba lakini wana makazi yaliojengwa vibaya. Msaada kidogo sana kutoka kwa famila au mtandao wa kijamii. Hawana uhakika wa mapato au wanategemea msaada kutoka kwa majirani. |


ZOEZI

## Kutambua vyeo vya ustawi au uzuri

Kama mwezeshi au Mwezeshaji ataonelea ni vyema pamoja na kundi linalohusika,fanya Zoezi hili; mpe kila mmoja nambari kwenye kijikaratasi cha kubandika bila jina. Kisha waulize wahusika wajiweke pahala wanajihisi wapo kwenye chati. Kisha waulize kama wanahisi wamejiweka katika kiwango/ cheo kinachofaa uliza maswali ili kuwahimiza kuhusika vikamilifu kisha tazama yayoendelea kwa uangalifu. Kisha uliza; unahusu vipi kulingana na pahala ulipojiweka binafsi?” Kisha pata makubaliano kutoka kwa kila mmoja kwamba wapo mahali panapo faa

Kuna uwezo wa kulifanya zoezi hili bila vitambulisho vya wahusika kwa kutumia mawe madogo madogo au mbegu kama vitambulisho vyao. Watu binafsi na nyumba au familia huenda zikasonga kwenda juu au chini katika vyeo hivi jinsi afya yao au mambo mengine yanavyobadilika.Hatua tofauti zitahitajika kushughulikia hali tofauti za udhaifu/mazingira magumu.

**KUMBUKA:** Zoezi hili linaweza kutumika mwanzo wa mafundisho ya riziki/maisha kama chanzo muhimu.



ZOEZI

## Mienendo

Uliza watu wafikirie hapo awali na matukio muhimu kati ya miaka mitano au kumi iliyopita. Chagua jambo ambalo watu wengi watakumbuka sana – Kwa mfano, ufunguzi wa kituo cha afya, uchaguzi wa mwanasiasa mashuhuri, au Ukame. Uliza watu mabadiliko ambayo yamefanyika tangu wakati huo na kufanya mambo yawe magumu. (Kwa mfano, kupungua kwa mazao, uwepo wa mafuta, bei ya soko ya mahindi,unyanyapaa unaohusiana na virusi vya Ukimwi. Hili litawasaidia watu kuelewa madhara ya mienendo kwa wakati fulani



*Ukame ni jambo ambalo huwatatiza watu wengi na huleta madhara makali sana. (Picha: Jim Loring / Tearfund)*

ZOEZI

# Kalenda ya msimu

Hili ni Zoezi muhimu sana linalohusisha wahusika na linasaidia katika kuonyesha habari muhimu kuhusu udhaifu wa watu/Mazingira magumu wakati fulani wa Mwaka. Kuchunguza mambo yaliyonakiliwa huenda yakaonyesha kwamba hatari zingine hutokea mara nyingi kila Mwaka. Mizunguko kama vile bei ya mimea au magonjwa yanaweza kubainika. Kwa muda wa miaka kadhaa mizunguko Fulani huenda ikatokea tena na kujadili matokeo haya kunaweza kuwapa watu motisha wa kufikiri kwa kina mizunguko hii.

Chora mfano wa kalenda ukionyesha aidha miezi iliyomo katika Mwaka kama unaishi mjini, au misimu ya mvua kama unaishi mashambani. Onyesha siku kuu kama vile Pasaka au Krismasi, majira ya mvua, majira ya mavuno na mihula ya shule kulingana na muktadha.

Kufanya Zoezi hili kwa makundi madogo kiasi cha watu wanne au wanane, wachangie mawazo tofauti ya aina tofauti za udhaifu/mazingira duni unao athiri maisha ya watu. Fikiria kuhusu mambo ya Kifedha ambayo huathiri familia katika mwaka, kama vile mapato tofauti ama mifano ya ulaji wakati Fulani wa mwaka. Chagua mifano muhimu ambayo athiri maisha ya watu na ambayo inayoweza kuwafanya wawe na udhaifu/mazingira magumu, kisha uyapange kwenye kalenda ya msimu uliyoiunda. Kwa mfano:

- Mapato ya familia
- Afya duni
- Usambazaji wa maji
- Wafanya kazi wa shamba wanaohitajika

| | MSIMU WA UKAME<br>Septemba Octoba Novemba | MSIMU WA UKULIMA (UMEKAUKA)<br>Desemba Januari Februari | MSIMU WA MVUA<br>Machi Aprili Mei | WAKATI WA MAVUNO<br>Juni Julai Agosti |
|---|---|---|---|---|
| MAPATO YA FAMILIA | 7 | 11 | 2 | 4 |
| MATUMIZI YA FAMILIA | 7 | 9 | 3 | 4 |
| UWEPO WA CHAKULA | 12 | 4 | 2 | 5 |
| MAGONJWA | 7 | 2 | 9 | 6 |

Gawia kila kundi mbegu au mawe madogo madogo.(ikiwa watu wanatumia miezi, tumia mbegu arobaini na nane. Kama watu wanatumia misimu, tumia mbegu ishirini na nne) tazama kila suala tena kisha ugawanye mbegu ipasavyo kwa kila mwezi ama misimu ya mwaka. Iwapo, kwa mfano, afya duni ni tatizo sana, weka mbegu nyingi katika sehemu hii. Katika miezi ambapo afya ni bora, tumia mbegu chache au usiweke zozote. Wakati mapato ya familia ni mengi, weka mbegu nyingi, wakati kuna upungufu wa mapato, weka mbegu chache. Himiza uwepo wa majadiliano. Wakati kila kalenda imekamilika, njooni pamoja kwa majadiliano na maelimisho kutoka kwa kila kikundi.

## Majadiliano


- **Tazama matukio muhimu ambayo hufanya watu kuwa katika mazingira magumu katika mwaka**
- **Je, mapato ya familia yanabadilika vipi katika mwaka? Athari zake kwa udhaifu/mazingira magumu ni yapi?**
- **Kunazo njia za kupunguza matatizo yanayoikumba familia katika misimu Fulani?**

- **Je, kuna matatizo yoyote ya kiafya katika nyakati tofauti katika mwaka?**
- **Je, kuna uhusiano wowote wa karibu baina ya masuala tofauti? Kwa mfano, watu kuwa na afya duni wakati ajira inahitajika sana kwa sababu wako na njaa.**

Kalenda ya msimu ina angazia uhusiano wa karibu baina ya udhaifu/ mazingira magumu na kuongeza ufahamu wa mambo yanayo pelekea watu kuwa dhaifu/mazingira magumu.

ZOEZI

## Hisia tofauti katika mwaka




Hili ni zoezi la hiari na laweza kufanyika baada ya kufanya zoezi la kalenda ya misimu.

Kutumia kalenda ya msimu (Kama ilivyochorwa hapo juu), wape wahusika vijikaratasi vitatu vya kubandika, kila mojawapo na zote zikiwa na picha ya sura ya binadamu – moja iliyo na tabasamu, nyingine hapo kati kati na nyingine iliyokosa furaha. Waulize wahusika watumie picha hizo kuonyesha jinsi wanavyohisi kuhusu masuala mahsusi nyakati tofauti katika mwaka. Ni lini watu huhisi furaha sana? Ni wakati gani wao hupatwa na wasi wasi kutokana na masuala mengine? Ni lini maisha ni sawa kabisa Kisha, waulize wahusika waweke sura zao katika chati ya msimu kama majibu kwa masuala kama vile:

- Matumizi ya mwaka
- Uwepo wa ajira
- Uhalifu
- Uwepo wa chakula

Matarajio ni kwamba, picha za sura zitaonyesha mitindo na mienendo na zitapelekea kuwepo kwa majadiliano mazuri. Uliza jinsi wahusika hukabiliana na mambo magumu wakati tofauti katika mwaka.

Jadili matokeo, Ni nini kinaweza kufanyika ili kubadili na kuboresha ugumu unaotokea nyakati tofauti katika mwaka.

# Uhimilivu/jinsi ya kukabiliana

Kama wahusika wanaweza kukabiliana vizuri na mambo magumu, tunasema "wamehimili" vizuri na waweza ukafafanua kuwa wao ni " mashujaa" ushujaa ni kinyume cha udhaifu/mazingira magumu; Huelezea uwezo wa kuwa na nguvu wakati kuna changamoto za maisha. Watu walio na uwezo mkubwa wa kufikia rasilimali watakuwa na uhimilivu sana wakilinganishwa na wale ambao hawawezi kufikia rasilimali. Kwa mfano, mkulima mvumilivu anaweza kuwa na akiba ya kununua chakula iwapo mimea haitakua kwa sababu ya ukame, muuzaji mvumilivi wa kibanda ingawa anaweza kupoteza mali yake kutokana na janga, bado atakuwa na uwezo na fedha za kutosha kununua bidhaa zingine na kuanza tena upya.

Ili familia iweze kupunguza udhaifu wake/mazingira ngumu kutokana na hatari, yapasa kuongeza uhimilivu. Hii inaweza kufanyika kwa kuongezea na kujenga rasilimali ilizonazo na kwa kuboresha uwezo wao wa kukabiliana/kuhimili nyakati ngumu

Kuna aina mbili za kuhimili/kukabiliana na mambo, (Chanya) vizuri au (Hasi) vibaya. **Kuhimili vizuri** (hulinda uwezo wa maisha/riziki) kunaashiria uwezo wa kulinda rasilimali muhimu. Aina za kuhimili mambo ni mbaya iwapo zitachangia hasara ya rasilimali na umasikini. Katika majanga yanayo dumu kwa muda mrefu, aina za kuhimili/kukabiliana nayo huenda yakawa na mikakati ya riziki/maisha (Kwa mfano, kuwafanya watoto wawe waombaji wa msaada barabarani au wafanya kazi)

Utathmini wa riziki/maisha unahitaji uchunguzi wa makini kwa mbinu za kukabiliana/kuhimili: kile haswa watu hufanya wakazi wa matatizo. Aina za jinsi ya kuhimili/kukabiliana na mambo hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine, na kutoka kundi moja hadi jingine, kwa hivyo mbinu zinazotumika kuhimili/kukabiliana zapaswa kuachunguzwa katika muktadha tofauti.

## Mifano ya mikakati chanya na hasi ya kukabiliana/kuhimili

### Mifano chanya ya kuhimili

- Kupokea mafunzo ili kupata kazi inayolipa vizuri
- upanzi wa mimea ili kupunguza matumizi yanayotokana na chakula
- Kuanzisha biashara ndogo
- kupokea matibabu ya bure kutoka kwa serikali
- kupokea msaada wa muda wa chakula kutoka kwa kanisa
- Kukodisha nyumba usizotumiaili kuongeza kodi
- kupata msaada kutoka kwa majirani haswa wakati wa mavuno
- ufugaji wa mifugo kama vile sungura n.k ili kuongeza mapatona kuboresha lishe

### Mifano ya kuhimili

- Kupunguza idadi ya vyakula
- Kununua chakula cha bei rahisi ama kisichokuwa na madini muhimu
- Wanafamilia kuhama wakitafuta kazi
- Kuuza rasilimali zisizozalisha kama vile mikufu n.k
- Kutoa watoto kutoka shuleni
- kujihusisha na vitendo vya ngono kama ajira
- Kuuza au kuchinja mifugo
- Kuuza rasilimali zinazozalisha kama vile ardhi ama vifaa vya ukulima

Baadhi ya njia mbaya za kukabiliana na mambo huenda ikaongeza hatari ya maambukizi ya Ukimwi kwa wana familia walio na afya bora. (Kama vile ukahaba, (mapatano ya ngono au ngono ya malipo na ajira ya Kuhama hama) Kutumia mwongozo huu kutasaidia kutambua mbinu zitakazo wawezesha kupunguza hatari ya maambukizi na kupunguza madhara ya njia hizi.

## 3 MASWALI YA MWONGOZO
## Mazingira magumu na njia za kukabiliana

MaNakili majibu ya maswali yafuatayo kisha uyajaze katika chati (Template) iliyo na **Maswali ya Mwongozo Sehemu ya 3** katika ukurasa wa 30. Majibu haya yaweza yakaachwa na wahusika wa kikundi au jumuia na mengine yakasalia na Mwezeshaji. Hivi, utaweza kufuatilia maswali muhimu na kisha baadaye yatakuelekeza katika mwongozo huu.

Maswali haya yatasaidia katika kutambua chanzo cha hatari na Kubaini jinsi wanaolengwa kwa mafundisho haya wanaweza kukabiliana.

Hakikisha ya kwamba maswali yote yameshughulikiwa. Iwapo umelifanya zoezi la kalenda ya msimu tayari, irejelee katika majadiliano na kikundi.

**3a** **Ukirejelea katika zoezi la kalenda ya msimu au "Zoezi la hisia tofauti katika mwaka", jadili hatari zote ambazo zimeikumba familia katika miaka ya hivi karibuni. Ni hatari zipi hutokea kwa ghafla? Ni hatari gani zaweza kutabirika? Ni hatari gani zimekuwa na uzito mkubwa katika miaka mitano iliyopita? Jadili madhara yake.**

Chagua hatari tatu ambazo zina madhara makubwa katika familia na kwa umuhimu wao.

Baada ya kuchagua hatari tatu zilizo na na umuhimu mkubwa kwa walengwa, Zingatia madhara yake kwa familia Ni nini kilifanyika baada ya kila hatari? Kwa mfano, mimea haikumea kwa sababu ya ukame, nyumba ziliharibiwa na maporomoko ya ardhi, watu waliugua magonjwa yanayotokana na mvua, au familia ilipoteza mali yote baada ya baba mwenye nyumba kufariki.



*Mifugo wadogo kama vile sungura ni rahisi kutunza haswawakati watu hawana nishati na nguvu. (Picha: Moses Kamau Wanjiru / Samaritan's Purse)*

### Mazingira magumu ya watu wanaoishi na Virusi Vya Ukimwi

Watu wanaoishi na Ukimwi huenda wakahitajika kurekebisha riziki/maisha yao ya sasa kwa vile huenda wakakosa nguvu au uwezo. Baadhi ya marekebisho muhimu huenda yakahusu yafuatayo:

**KAZI ZA USANIFU:** Kazi za nyumbani kama vile. kushona na kutengeneza vikapu zinahitaji nguvu kidogo kushinda kazi za mkono.

**KUWEKA MIFUGO:** Kutotilia mkazo kwa mifugo kama mbuzi na kuwa makini zaidi na mifugo kama sungura, na kuku ambao ni rahisi kuwatunza na wanaweza kuwekwa karibu na nyumba

**KUTEUA MAZAO:** Kufanya majaribio ya mimea inayohitaji muda mchache wa matunzo ama mimea iliyo na faida kubwa ya pesa au madini. Mfano ni kama vile mizizi inayotumika kama mafuta ama chakula. Kusambaza mavuno katika misimu tofauti kutasaidia katika kuepuka kuhitajika kwa ajira kubwa.

Yapitie maswali yafuatayo moja kwa moja kwa kila athari tatu tofauti zilizochaguliwa.

**3b** **Je, familia zimekabiliana vipi na hatari tofauti? Jadili njia zote ambazo watu hukabiliana na hatari tofauti. Kisha jadili njia chanya (Positive coping) za kukabiliana na hatari na zilizo hasi(Negative coping)**

Kwa mfano, uliza watu ni mambo yapi wao hufanya wakati hatari zinatokea (yaweza kuwa ukame, maporomokoya ardhi, Ukosefu wa ajira na kadhalika.) Nakili njia zote ambazo watu hukabiliana na hatari. Jadili njia note nzuri kukabiliana na zile ambazo si nzuri.

Unaweza kugawanya kikundi mara mbili, kisha elekeza kikundi kimoja katika kujadiliana njia bora za kukabiliana na kundi jingine lijadiliane njia ambazo si bora katika kukabiliana na hatari. Baadaye, leta makundi yote mawili yaje pamoja ili kuafikiana katika majibu yao.




*Migombahuathiriwasana na hatari kama vile – ukame, upepo mkali na magonjwa au wadudu mbali mbali (Picha: Moses Kamau Wanjiru / Samaritan's Purse)*

**3c** **Je, watu wengine kutoka kwa jamii wameweza kukabiliana vizuri? Kwa nini?**

Je, hatari hizi ziliwaathiri watu wengine kutoka kwa jamii husika? (Ama jamii zingine) wao walikabiliana vipi na hatari hizi? Walikuwa na uwezo mkubwa wa kuwawezesha kukabiliana vizuri? (Walistahimili zaidi) Kama ndiyo, walikabiliana vizuri vipi ?

**3d** **Ni nini kinaweza kufanywa ili kusaidia familia kukabiliana vizuri na majanga katika siku zijazo?**

Je, utafanya nini ili kukabiliana vizuri zaidi wakati majanga/hatari zinatokea? Utawezaje kuchukua hatua ya kuzuia kuingiza familia yako katika hatari? Angalia jinsi gani watu wengine wameweza kukabiliana (Swali 3c). kisha angalia kama unaweza kutumia majibu yao mazuri.

Kwa mfano, unaweza kupendekeza uwezekano wa kupoteza ajira kama athari mojawapo. Matokeo yake huenda yakawa mapato ya chini, chakula kidogo na kukosa kujiamini. Mtu anaweza kukabiliana vibaya, Kwa kupiga mtindi, kuongeza madeni au kutoa watoto shuleni. Wanaweza kukabiliana vizuri kwa kupata ushauri, na msaada wa kuanzisha biashara ndogo kando kando mwa barabara. Wengine waliopoteza ajira katika jamii hutafuta mafunzo na kuchukua mkopo mdogo ili kuanzisha biashara ya kurekebisha baiskeli zilizoharibika. Familia zinaweza zikasaidiwa katika siku za baadaye kuanzisha vikundi vya hazina na kuboresha uhusiano na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) yanayotoa mafunzo anuwai.

MASWALI YA MWONGOZO YA SEHEMU YA 3

# Mazingira magumu na njia za kukabiliana

| **3a** Andika hatari tatu ambazo zimekuwa na madhara mengi katika familia | **3b** Je, familia zimekabiliana na hatari hizi vipi? Nakili njia nzuri na mbaya za kukabiliana | **3c** Je, watu wengine kutoka kwa jamii wameweza kukabiliana vizuri? Kwa nini? | **3d** Je, nini kinahitajika ili kusaidia familia kukabiliana na hatari vizuri? |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

SOMO LA NNE

# 4 Taasisi, sera na michakato ya sera

Taasisi, sera na michakato ya sera (PIPS) zinaweza kuchukuliwa kama sheria na taratibu zinazoathiri maisha ya watu. Haya ni mambo kama vile: kijamii, kisiasa, kiuchumi na kitamaduni katika mazingira ambamo watu huishi na kufanya kazi.

Sera, taasisi na michakato ya sera ni pamoja na sheria, kanuni, taratibu, utamaduni, mila na mifumo inayoathiri na kuthibiti maisha ya watu. Hujumlisha taasisi na mashirika ya serikali na yasiyo ya kiserikali ambamo lengo lao ni kutoa huduma kwa kushughulikia mahitaji ya watu wanaoishi katika mazingira magumu. Sera, taasisi na michakato pia huathiri upatikanaji wa mali, jinsi mali mbalimbali zinaweza kutumika kuzalisha riziki na aina ya misaada ambayo watu wanaweza kupata.

Vile vile, zina jukumu muhimu katika kubadilisha maisha ya watu. Hata hivyo sera, taasisi na michakato ya sera husahaulika mara nyingi lenzi ya riziki inapoangaziwa. Lenzi nzuri ya riziki itaangazia msingi, mageuzi na ushawishi wa sera , taasisi na michakato ya sera ili ziweze kutoa huduma ya maisha bora wa kundi lengwa.

Hali kadhalika,sera, taasisi na michakato zinahusu masuala muhimu ya uongozi, haki na utawala bora. Huwa zinashughulikia mizizi ya matatizo yanayo wakabili watu wanaoishi katika mazingira magumu. (Kwa mfano, Unyanyapaa, ubaguzi, na usawa wa kijinsia na kadhalika) Vile vile zinaweza kuwa na athari kubwa juu ya masuala ya haki ya jamii na heshima ya binadaamu.

Shughuli hizi ni muhimu sana haziwezi kudharauliwa!

Je, ni aina gani ya sera, taasisi na michakato ambazo tunazungumzia? Majedwali yafuatayo yameorodhesha baadhi ya mifano ya kila moja.

## Sera
## (Sheria na kununi)

Sera ni kama nia, mipango ya utekelezaji ya serikali, shirika au mtu binafsi. Wakati mwingi sera hufanywa thabiti kama sheria na kanuni au sheria zinazoathiri maisha yetu. Baadhi zinaweza kuwa ni kanuni zinazoongoza upatikanaji wa mikopo na ardhi.

Kwa mfano: Tafakari:

- Nini inahitajika nchini mwetu ili mtu aweze kupiga kura au kumiliki mali?
- Je, sheria inasemaje juu ya urithi katika nchi yetu? Je, Sheria inafuatiliwa?

### Baadhi ya mifano ya sera

**SERA ZA FAMILIA**

- Haki ya urithi
- Umiliki wa ardhi.

**SERA ZA JAMII**

- Kanuni zinazoamua jinsi ya kupata ardhi, maji na misitu.
- Mamlaka ya viongozi kutunga sheria.


**SERA ZA KANDA, UKOO AU WILAYA**

- Kanuni zianazosimamia usambazaji wa chakula.
- Soko za mazao ya chakula.

**SERA ZA KITAIFA**

- Watoto wote wana haki ya elimu ya msingi.
- Waathiriwa wa virusi vya Ukimwi wana haki ya kupata dawa za kupunguza makali bila malipo.
- Wanainchi wote wana haki ya uwakilishi wa kisheria.

# Taasisi (Miundo au mashirika)



Utangulizi mwafaka wa dhana ya taasisi ni kuuliza watu wawaze kuhusu pahali wanapoenda wanapokumbwa na tatizo, hitaji, wanapopata shida Fulani itatuliwe au wanapohitaji mawaidha. Hizi zinaweza kuwa afya, masomo, kazi, fedha au masuala ya kisheria.

### Baadhi ya mifano ya taasisi

**TAASISI ZA KIJAMII**

- Mashirika ya kiraia
- Hospitali na kliniki za jamii
- Huduma za ugani
- Mashirika ya benki na mikopo
- Miundo ya utawala k.m Chifu au serikali za mitaa
- Vyama vya ushirika wa wakulima
- Vikundi vya wamama vya akiba na mikopo.
- Vikundi saidizi vya wajane
- Shule
- Kliniki na hospitali
- Maduka ya mitaa na biashara
- Kampuni za usafiri
- Ukoo / Kabila

**MASHIRIKA YA KIROHO**

- Kanisa
- Misikiti
- Ushirika wa nyumbani
- Vikundi vya kusoma vitabu vitakatifu
- Kamati za kanisa

**TAASISI ZA KIUCHUMI**

- Benki
- Taasisi ndogo za fedha (MFIs)
- Wakopeshaji pesa
- Soko
- Kampuni za usafiri

**TAASISI ZA KISIASA**

- Vyama vya kisiasa na bunge
- Vyama vya sheria na mahakama
- Polisi
- Bodi ya ardhi
- Wizara za serikali – ardhi, jinsia, elimu, kilimo
- Viongozi wa kijiji

## Vikundi vya kujitegemea na sera na taasisi na michakato

Vikundi vya kujisaidia (SHGs) hutoa mfano mzuri wa taasisi inayonufaisha. Kila kundi lina kanuni zake na michakato ambayo huundwa na kukubaliwa na wajumbe. Kila chama hutoa sera zake kwa mfano Kanuni kuhusu mikopo na malipo kwa wanachama.

Vyama hivi vinaweza kuwa na uhusiano wa karibu na taasisi ndogo za kifedha za kusaidika na raslimali za taasisi hizi kama vile huduma za benki na malipo.

Vyama vya kujisaidia vinaweza kupata mawazo mazuri kutoka kwa serikali za mitaa huku zikinufaika kwa sera ambazo zinaweza kutoa huduma, ushauri au kuviunganisha kwa taasisi zingine. Kwa mfano Vyama vinaweza kuunganishwa na serikali za miji ambazo zinaweza kutoa huduma za fedha na rasilimali ili kuwawezesha kupanda miti katika maeneo yaliyoathiriwa kwa ajili ya ulinzi wa mazingira.

# Michakato (Mifumo na desturi)

Michakato ya sheria zisizoandikwa hushawishi mifumo ya ndani, kanuni za kitamaduni, taratibu za kijamii, familia, mila na desturi za kidini.

Zinahusu jinsi maamuzi hufanywa,na kama yanafanywa kwa maslahi ya jamii nzima au maslahi ya wenye mamlaka tu. Baadhi ya sera na taasisi hushindwa kukidhi mahitaji ya wanaoishi katika mazingira magumu.

Kwa Mfano: Je, maamuzi hutolewaje katika jamii? (Nyumbani au wilaya) na je, ni nani anayehusika katika michakato? Je, ni michakato gani muhimu ambayo wasindikaji wa chakula wanapaswa kufuata?(usafi, chakula kizuri cha hali ya juu, au ufungaji wa bidhaa

Je, ni utamaduni mila au mazoea yapi yana athiri maisha ya wanawake? (Vurugu za kijinsia, kurithi kwa wajane, mahari?)

Je, ni michakato ipi inawezesha mtu kuwakilisha jamii yake katika wilaya au taifa kama mbunge? (Mifumo ya kisiasa?)

Je, kuna aina gani zinazosaidia watu kupata ushauri wa kisheria au kuwakilishwa?

### Baadhi ya mifano ya michakato

**MICHAKATO YA FAMILIA**

- Imani kwamba watoto wa kike hawana haja na elimu
- Wanaume hufanya maamuzi yote ya kifedha ya familia

**MICHAKATO YA KIJAMII**

- Imani kwamba wanawake hawapaswi kupanda baiskeli au kufanya baadhi ya kazi
- Wasiojua kusoma na kuandika huteseka kujaza karatasi zinazohitajika ili kupata huduma za afya
- Uchaguzi wa kijiji / baraza la jamii

**MICHAKATO YA KANDA, UKOO AU WILAYA**

- Mikutano ya jumuiya / kijiji
- Ruzuku za wakulima wa kahawa
- Ruzuku za zana za pembejeo kwa wakulima hohe hahe
- Mikopo ya miradi kwa ajili ya wakulima kuhamasisha wawekezaji katika zana
- Wasiozungumza lugha ya kingereza kuwa na hofu ya mbinu za kuomba misaada kwa mashirika yasiyo ya kiserikali. (NGOs)

**MICHAKATO YA KITAIFA**

- Uchaguzi wa kitaifa wa urais
- Mifumo / michakato ya kisheria
- Ardhi na madai ya kumiliki ardhi
- Mchakato wa kusajili kuzaliwa.

# Jinsi ya kutumia michakato, sera na taasisi ili kutoa changamoto katika mitazamo mibovu ya kijinsia

Mila na desturi nyingi za jadi zina thamani na uwezo mwingi.Lakini wakati mwingine zaweza kutosaidia kamwe. Hata hivyo, sheria mpya zinaweza kutoa changamoto kwa desturi na mitazamo hiyo. Sasa hebu someni misemo ifuatayo kuhusu jinsia. Ongezeni baadhi kutoka kwa tamaduni zenu kisha mjadili misemo hiyo. Je, kila moja ina maana gani? Inaonyesha msimamo au mtazamo upi? Je, waweza kufikiria kuhusu sera, taasisi na michakato ambayo itatoa changamoto kwa maoni yasio ya faida?

*"Wanawake waweza zaa watoto werevu lakini wao si werevu."*

*"Uamuzi wa mwanamke huwa si wa kweli kila wakati. Haaminiki."*

Yote Hii ni mifano ya mithali za kitamaduni

## Shinikizo la kifamilia

Penina alikuwa na watoto wanne na aliishi karibu na Lira, Uganda kaskazini. Pindi mumewe alipofariki wakwe zake walimnyang'anya ardhi. Naye akaenda kanisani kuomba msaada. Washirika wakaamua kwenda katika korti la baraza la migogoro ya ardhi.

Hata hivyo, wakwe zake Penina waliposikia vile, wakamweleza kuhusu sheria ya ukoo inavyosema. Wakamwambia, "Mwanamke hana haki ya kumiliki ardhi; kwa hivyo sisi tunataka kulinda ardhi kwa sababu ya watoto wako." Kwa hofu ya kukataliwa na jamii, Penina alikubaliana nao na hakuiendeleza kesi yake.

Kufuatia hayo, jumuiya ya kanisa haingefanya lolote kwani Penina hakutaka kwenda kinyume na familia yake. Watu walibaki kulinda ile ardhi huku wakiwakumbusha watoto kuwa ile ardhi ilikuwa yao.

**SUALA LA KUJADILI** Je, ni jambo gani linaweza kufanywa ili Penina asaidike?

*"Kumwamini mwanamke ni kama kuamini ukungu."*

*"Moyo wa mwanamke nidhaifu kama titi lake."*

Mithali ya kitamaduni

### Mikakati chanya ya kuathiri sera, taasisi na michakato

Kuna idadi kubwa ya mikakti ambayo inaweza kuathirisera ,taasisi na michakato na kusaidia watu kupata maisha yaliyo na uendelevu. Yafuatayo ni baadhi ya mawazo:

- Kuelimisha watu kuhusu haki zao za kupata afya bora, masomo na huduma za misaada hasa kwa wanaoishi na virusi vya Ukimwi.
- Kuunganisha watu kwa taasisi zinazotoa mafundisho na misaada riziki
- Kurejesha utamaduni wa kusaidiana kikazi na ukulima wa jamii
- Kushawishi kwa haki za urithi wa wajane na yatima
- Kukuza upatikanaji wa huduma za ugani kwa wanaoishi na virusi na jamii zilizoathirika
- Kupambana na unyanyapaa na ubaguzi kwa wanaoishi na virusi vya Ukimwi na jamaa zilizoathiriwa.
- Kuongeza upatikanaji wa mikopo kwa miradi ya wajane, wazee na yatima.
- Kutoa misaada ya mikopo kwa taasisi ya mikopo katika jamii.



*Picha: Kutayarisha chakula cha kuuza kunahitaji ufahamu wa sera, taasisi na michakato kuhusu usafi wa vyakula. (Picha: Moses Kamau Wanjiru / Samaritan's Purse)*

# Haki za urithi

Kwa mara nyingi walioachwa katika jamiii wanaweza wakapoteza sio tu waume / baba zao lakini ardhi na nyumba zao. Pia mifugo na mali zingine kutokana na desturi za urithi katika jamii. Kuandika wosia kuchagua mlezi hali kadhalika kupata ushauri wa kisheria kuhusu urithi maisha na kubaki salama baada ya kifo cha mume/mke na watoto wa marehemu. Michakato hii itasaidia kuhakikisha wanaweza kushikilia mali muhimu ambayo itawasaidia kudumisha maisha na kubaki salama baada ya kifo cha baba /mume.

**DOKEZO LA MSAADA:** Huenda ukapata kwamba mambo yanaingiliana unapokuwa unapozingatia sera, taasisisi na taratibu. Kwa Mfano, Ukosefu wa sheria zinazolinda haki za miliki za wajane huweza patikana katika sera za kitaifa, taasisi za kisheria ama taratibu za kisheria ambapo kila suala linaonekana la muhimu.

*"Sasa watu wameunganishwa na marafiki, wazee wa kijiji na serikali. Iwapo serikali itatufahamu vizuri,hii itasaidia. Sasa tunajua mahali pa kupata usaidizi."*

Aliyenufaika na mafundisho haya

## Watu wenye mamlaka!

Watu wenye mamlaka wakati mwingine wanaweza kuathiri sera taasisi na taratibu. Wanaweza kuamua

- Watu watakao pata mali na huduma
- Nani anayepata ujumbe muhimu na ni nani asiyepata
- Anayehusika katika utoaji wa maamuzi na ni nani asiyehusika.

Watu, vikundi ama jamii iliyo na mali (iwe ya kifedha, kimwili, kijamii au kisiasa) mara nyingi huwa na ushawishi na hudhibiti sheria ya mashirika yaliyo karibu nao.

Watu walio na uchache wa mali au ujuzi wanahitaji msaada ili kuepuka umaskini wao na kutambua mbinu na taasisi ambayo inaweza kuwasaidia kupata haki na misaada ya kijamii.

ZOEZI

## Mitandao ya kijamii


Wazazi wa watoto watatu wameaga dunia kutokana na magonjwa yanayohusiana na Ukimwi, wameacha kifungua mimba fatuma aliye na umri wa miaka 14 kama mkuu wa nyumba na ndugu mmoja na dada mmoja. Uliza mshiriki mmoja asimame katikati mwa chumba ili amwakilishe Fatuma. (Mpatie jina linalojulikana na wote)

Waombe washiriki wamzingire Fatuma mmoja baada ya mwingine wakati zoezi likiendelea. Himiza kila mmoja ashiriki kuchagua pahali watu wanapaswa kusimama. Je nani aliyekaribu na Fatuma? Ni nani atakayempatia msaada? Chagua washiriki wengine wawakilishe nduguye Fatuma, dada na nyanya yake aliyekaribu. Je, nani mwingine anayefahamika na Fatuma? Ni nani mwingine Fatuma anaweza kumfikia kwa msaada au ushauri?



Tenga mjomba wake Fatuma anayeishi mji unaokaribia mbali kidogo. Hebu mchungaji wa kanisa asimame pahali mjomba wake alipo aliye na marafiki ambao hufanya kazi katika shirika lisilo la serikali ambalo hutoa mafunzo kwa watoto walio katika mazingara magumu. Rafiki huyu asimame mbali kiasi. Endelea kwa kufuata mapendekezo kwa kuwaambia washiriki wote wasimame wakiwakilisha mashirika na watu tofauti.

Kama wanahusiana na wanatoa msaada wasimame karibu. Lakini




kama watu wana uwezo tu wa kusaidia wasimame mbali zaidi.

Je, Fatuma anaweza kuchukua hatua gani kusaidia jamii yake iliyo katika mazingara magumu – Ndugu na dada zake wachanga? Ni ushirikiano upi unaoweza kusaidia kujua sera, taasisi na michakato ya umuhimu? Je, ni mbinu zipi zinazoweza kusaidia jamii yake kusonga mbele?

Sasa hamisha kundi hili la watu katika chati – huku ukitaja kila mtu na shirika. Katika kufanya zoezi hili umeunda mtandao wa kijamii kwa msichana huyu, chora mistari kozo kwa uhusiano (wenye nguvu).


Mistari nyembamba kwa uhusiano dhaifu na

Mistari nusunusu kwa uhusiano unaoweza kuchipuka

Mitandao ya kijamii inaweza kutumika kubaini uhusiano na watu wenye uwezo mkubwa na kuchora ramani ya kila aina ya viungo vingine kati ya makundi ya watu, taasisi na mashirika ambayo inaweza kuwa na athari chanya na hasi. Mtandao ya kijamii inatumiwa kuonyesha uhusiano. Michoro ya 'venn' na 'spider' inaonyesha uhusiano kati ya kaya na mashirika.

Michoro ya 'venn' hutumia duara zinazopishana kwa ukubwa ili kuonyesha umuhimu na uhusiano wa mashirika tofauti. Mchoro ufuatao unaonyesha uhusiano ambao kaya maskini katika jamii iliyo nchini Swaziland na taasisi za mitaa mila na wakala wa serikali.

## Uhusiano kati ya utumizi wa ardhi na sera, taasisi na michakato.



Sasa chora mtandao jamii (kwa uhusiano mchoro wa chapatti (Venn) au wa bui bui (spider) unaonyesha uhusiano na taasisi. Kwa kikundi ulichounganisha nacho (K.M chama au chama cha kuweka akiba au cha wamama) ili kujibu maswali yanayofuata zoezi hili litasaidia kujibu swali la 4b hapa chini.

MASWALI YA MWONGOZO

# 4 Sera taasisi na michakato

Maswali haya yameundwa ili kuwasaidia washiriki kutambua hali zao kuhusu sera, taasisi na michakato. Pia waanze kutambua na kutoa kipau mbele kwa baadhi ya ufumbuzi wa matatizo yao wenyewe.

Linganisha majawabu yaliyotolewa kwa mazoezi yaliyonyesha taasisi sera na michakato na athari za watu na vikundi.

Wakati washiriki wakijibu maswali haya, rekodi majibu yao katika chati. Pia, jaza nakala za **Maswali ya Mwongozo ya Sehemu ya 4** katika ukurasa 39. Majibu yaliyo katika chati yanaweza achwa kwavikundi lakini au jamii, majibu katika majedwali yatabakia kwa mwelekezaji. Hii husaida kuhifadhi majibu ya muhimu na elekeza kwa michakato ya baadaye.

**4a** **Tambua rasilimali mbili au tatu ambazo hazitumiwi vizuri na nyumba au kikundi chako (kama vile ardhi, ujuzi au upatikanaji wa mikopo)**

**4b** **Ni mashirika na taasisi gani yanayosaidia au kuzuia upatikanaji wa mali?**

Chora mchoro unao onyesha taasisi zote na mashirika ambayo yanasaidia kundi lako kupata mali. (Tumia orodha iliyo katika ukurasa 32) Basi kwa kutumia rangi tofauti chora taasisi na mashirika yote yanayozuia kundi lako kupata mali.

Kwa mfano: Je, ni shirika lipi kati ya haya mnafanya nalo kazi kwa karibu sana? Ni aina gani za huduma wanazotoa? Labda baadhi ya taasisi zinasababisha matatizo kwa kazi zenu – Kwa mfano;

Shirika lisilo la kiserikali linatoa taaluma bure na kuhamasisha utegemezi

- Vyama vya kisiasa
- Wizara za serikali (kilimo, afya, elimu)
- Mashirika yasiyo ya serikali, vyama vya kiraia, mashirika ya uanachama
- Kanisa, misikiti na taasisi za dini
- Shule, hospitali na huduma zingine za kijamii
- Mashirika madogo ya fedha
- Mifumo ya utawala wa jamii (wazee wa kijiji na chifu)
- Biashara na kampuni.



*Maisha ya mjini huongozwa na sheria, kanuni na sera nyingi. (Picha: Moses Kamau Wanjiru / Samaritan's Purse)*

## 4c Sera na michakato inayosaidia na isiyo saidia

Kisha tazama kila taasisi na mashirika na uongeze sera (sheria zilizoandikwa) au michakato yoyote (Sheria ambazo hazija andikwa) inayowasaidia unaowalenga kufikia rasilimali hii. (Ni rahisi kuandika haya katika kijikaratasi kilicho na gundi na kubandika pamoja)

Rudia hivi kwa kila taasisi na mashirika, wakati huu ukiandika sera na michakato inayowazuia unaowalenga kufikia rasilimali.

## 4d Je, ni watu gani wenye mamlaka?

Sasa chora picha ya mtandao wa kijamii wa kundi unalolenga (Tumia msingi wa mfano ulioutumia na fatuma) ili kubaini watu wenye mamlaka.

## 4e Sasa unda hatua, ni hatua gani wahusika wanahitaji kusonga mbele?(Rejelea ramani ya mtandao wa kijamii kubaini watu muhimu wanaoweza kuwaunganisha na watu wenye mamlaka)

Andika kwenye chati hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kuboresha ufikiaji wa rasilimali. Tengeneza hatua itakayochukuliwa kwa kila sera, taasisi na michakato inayozuia ufikiaji wa mali na pia hatua zinazoweza kuboresha ufikiaji wa sera, taasisi na michakato inayosaidia. Je, ni mtu gani au shirika lipi linaweza kushawishi ufikiaji kwa kundi unalolenga?

**DOKEZO LINALOSAIDIA** Inaweza kuwa muhimu sana kurudia zoezi zima kwa kuchagua rasilimali tofauti ili kuimarisha mafunzo. Iwapo unalifanya zoezi hili katika jamii unaweza kuchagua rasilimali tofauti ambazo hazitumiwi vizuri. Pitia maswali yote yanayohusiana na kila rasilimali ili uweze kubaini sera, taasisi na michakato zinazosaidia au kuzuia utumizi warasilimali hizi.

### Vijana katika jiji la Nairobi wamekosa maamuzi ya chaguo za riziki

Kundi moja la kikanisa linalofanya kazi katika vitongoji duni jijini Nairobi limegundua kwamba Kukosekana kwa maamuzi ya riziki kwa kizazi kichanga kumepelekea vijana wengi Kujiunga na makundi haramu na kutumia Madawa ya kulevya, na kuongezeka kwa visa vya unajisi na ngono ya malipo kati ya wavulana na wasichana. Haya yote yamechangia kuongezeka kwa maambukizi ya Ukimwi miongoni mwa vijana.

MASWALI YA MWONGOZO YA SEHEMU YA 4

# Sera, taasisi na michakato

| **4a** Rasilimali zisizotumiwa vizuri na kundi lako | **4b** Je, ni taasisi na mashirika yapi yanayosiadia au kuzuia ufikiaji wa rasilimali. | **4c** Sera na michakato inayosaidia na isiyosaidia | **4c** Je, ni kina nani wana mamlaka? | **4e** Je, ni hatua gani zinahitajika ili kusonga mbele? |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

SOMO LA TANO

# 5 Mzunguko wa thamani



*Usindikaji wa vyakula kama vile samaki kunaongeza thamani yake. (Picha: Moses Kamau Wanjiru / Samaritan's Purse)*

UUzaji wa bidhaa na huduma unaweza tazamwa kama mchakato au mfumo na hivyo basi huingia chini ya taasisi, michakato na mashirika. Hata hivyo, soko ni sehemu muhimu sana ya maisha hivyo basi tutazame mzunguko wa thamani sasa.

Hali ya kuwezesha watu kubadilisha mali zao za nyumbani kuwa bidhaa au huduma ambazo huingia katika mfumo wa soko hutoa mapato yaliyo na manufaa. Kila mtu anatakiwa kufikiria ambapo maisha yake yanaingia katika mnyororo wa thamani. Mara nyingi kuna uwezekano kuwa njia nyingi za kuongeza thamani ya bidhaa kwa kuzizongesha hatua moja au mbili ili kutoa thamani.

## Je, mzunguko wa dhamani una maana gani?

Bidhaa, mazao na huduma huingia sokoni katika hatua mbalimbali. (Angalia sanduku)

Katika kila hatua bidhaa hupata thamani. Bidhaa zilizotengenezwa hupata thamani kubwa zikilinganishwa na zizizotengenezwa. Bei katika maduka makubwa ama soko la kitaifa huwa juu kuliko soko la kawaida. Kuelewa kuchambua mzunguko wa thamani kutasaidia watu kuona kwamba njia ya kuongeza thamani ya bidhaa zao kwa kuzisongesha katika mzunguko wa thamani au kutoa mojawapo wa viungo.

### Watendaji katika mzunguko wa thamani

**WAUZAJI WA PEMBEJEO** Mwanzo, malighafi au pembejeo zinahitajika na yeyote anayewasilisha bidhaa. Hizi zinahusu mbegu, maji, mafundisho au vifaa vya hila.

**WAZALISHAJI** Pembejo hutumika kuzalisha mali ghafi kabla ya kusindika. Wazalishaji wanaohusika na shughuli kama vile: kupanda, kupalilia au kuvuna ili kuzalisha malighafi kama vile nafaka au mbegu. Kwa mara nyingi, wazalishaji huwa wakulima. Uzalishaji unahusika na kuzuia wadudu, kupaka nguo rangi, kuvuna maembe au kupokea maziwa, Usindikaji wa mianzi ya kufuma vikapu na kadhalika. Mali ambayo haijasindikwa inaweza kuuzwa hapa.

**WASINDIKAJI** Hatua inayofuata inahusisha kusindika mali hii katika njia tofauti. Kwa mfano, matunda yanakaushwa au yanatumiwa katika kutengeneza juisi au jemu. Mbegu za kahawa zinaweza kugandishwa, kukaushwa au kubondwa.Maziwa yanaweza kutumika katika kutengeneza jibini au maziwaya mgando. Nyama ya sungura inaweza kuchomwa.mianzi inaweza kufuma vikapu. Mali yote hii inatokana na wasindikaji. Hata hivyo, si bidhaa zote husindikwa. Kwa mfano, mandizi yanaweza kukaushwa lakini pia yanaweza kuuzwa moja kwa moja kwa wanunuzi.

**WANUNUZI NA WAUZAJI** Bidhaa kutoka kwa wasindikaji au wazalishaji zinaweza kuuzwa au kusambazwakwa njia tofauti. Zinaweza kuonyeshwa na kuuzwa katika soko la mtaa. Zinaweza pia zikafungwa vizuri na kuuzwa na Wanabiashara wadogo au Maduka ya jumla kwa soko la kitaifa. Utangazaji wa bidhaa utaongeza mauzo.

**WATUMIAJI WA MWISHO** katika mzunguko wa thamani, watumiajiwa mwisho ni wale wanaonunua bidhaa za kutumia au za kula. Wateja wanaweza kuwa watu wa mtaa, kitaifa au hata kimataifa.

ZOEZI

# Mchezo wa mzunguko wa thamani

Eleza kikundi wachague sekta iliyo na bidhaa wanazoweza kujitambulisha nazo (kama vile mbegu za alizeti, maziwa au ndizi) tambua wahusika wote katika mzunguko wa thamani: kwa mfano, wauzaji wa pembejo, wazalishaji, wakulima, wasindikaji, wasafirishaji, wauzaji wa kitaifa, wauzaji wa nje ya nchi hadi kwa mnunuzi wa mwisho. Kunaweza kuwa na mizunguko tofauti na soko tofauti, kwa hiyo ni vyema kuwa na mizunguko tofauti.

Chagua angalau watu watano kutoka kwa kikundi kuwakilisha wahusika tofauti katika mzunguko wa thamani. Waambie watengeneze mzunguko ndani ya chumba cha majadiliano. Iwapo uko na ndizi au embe, litumie lakini kamahapana, chora picha ya embe kwenye kijikaratasi. Kisha waulize wahusika (Wanaoigiza) kusongeza bidhaa mbele katika mzunguko. Hili linapoendelea, waulize waeleze thamani wanayo ongeza katika bidhaa ile.


Shughuli hii inapoendelea, chora mzunguko wa thamani kwenye chati (Tazama mfano wa mzunguko wa thamani ya kahawa hapa chini)

## Mzunguko wa thamani wa kahawa katika nchi ya uhabeshi

Wakulima wa kijiji nchini Ethiopia huzalisha kahawa) (Wao huuza katika soko la ndani kwa mawakala wa kijiji ambao hupeleka mbegu za kahawa katika kiwanda cha kusindika na kukaanga kutoka hapa, zinahifadhiwa na kupelekwa katika soko la kitaifa la kahawa katika mji wa Addis Ababa)

Kuna sheria (sera, taasisi na michakato) ya kudhibiti hatua zote tofauti ili kuhakikisha matokeo bora.Kufuatia uchambuzi wa mzunguko wa thamani, wanachama wa kundiwalitambua kulikuwa na fursa kwa kila mkulima kusonga mbele katika mzunguko wa thamani badala ya kila mkulima kuuzia wakala, wanachama wa kundi wananua mazao yote ya kahawa na kuyapeleka moja kwa moja katika kiwanda cha kusindika. Jambo hili lilihitaji fedha nyingi na mpangilio bora lakini lilichangia kupatikana kwa faida nyingi mno kwa kasi. Wanachama wa kundi walikuwa kasha songa hatua mbele katika mzunguko wa thamana.

**Jinsi mfumo wa uuzaji kahawa unavyofanya kazi katika nchi ya Uhabeshi**



Sasa unaweza kuuliza kikundi jinsi ya kufanya mzunguko wa thamani kutenda kazi kwa ushirikiano (kwa mara nyingi hii itakuwa katika kiwango cha uzalishaji)

- Je, kuna masoko tofauti ya kuuza bidhaa?
- Je, kuna njia mbalimbali wanazoweza kupata mbei nzuri ya bidhaa zao?
- Je,kuna njia ambayo kikundi kinaweza kusindika bidhaa ili kuongeza faida?

## Jinsi mzunguko wa thamani una fanya kazi

Kwa kuangalia undani katika mzunguko wa thamani ambao riziki za washirika hushiriki, tunaweza kuona jinsi thamani inaweza kuongezwa kwa matokeo yao na kuyasindika.Kama gharama ya usindikaji iko chini ya dhamana iliyoongezwa, basi lazima faida iongezeke. Kila mzunguko wa thamani huwa tofauti. Kila moja huwa na bidhaa mbalimbali, hatua mbalimbali, maeneo na soko mbalimbali.

Kuna uwezekano wa kuongeza faida bila uhifadhi.Kwa kuhifadhi mali ghafi kwa muda mfupi, muuzaji anaweza kujipatia faida kwa kuuza bidhaa msimu usio wa bidhaa hiyo.

Soko mbadala (mara nyingi mbali kidogo na soko la kawaida) linaweza kwa kiasi kikubwa kuongeza faida. Uuzaji unaweza kufanywa moja kwa moja na wazalishaji au wasindikaji. Hata hivyo kiasi kikubwa cha bidhaa na ubora wa bidhaa hulingana na mahitaji ya uuzaji. Katika hatua hii, majina ya bidhaa pia hutajwa.

**Kuelewa mahitaji ya wateja ni muhimu kwa kuelewa ni bidhaa zipi zitakazonunuliwa. Hata kama bidhaa ni bora kabisa haina thamani kama haina mnunuzi.**

Thamani ya bidhaa pia huathiriwa na pahali inapouzwa. Kuuza bidhaa kwa soko mbadala(mara nyingi mbali kidogo na soko la kawaida) kunaweza kuongeza faida sana. Kwa kushirikiana (pasipo na kushindana) Katika kununua pembejeo na kuuza bidhaa,wazalishaji wanaweza kupata bei nzuri na kuongeza faida. Kwamfano Maua ya alizeti yanakuzwa katika kijiji cha Lira.uganda

### Kila mhusika anaongeza thamani katika bidhaa...



**MALIGHAFI** (Wazalishaji)
- Maembe mabichi
- Maziwa
- Mianzi ya kutengeneza kikapu

**MALIGHAFI** (Wasindikaji)
- Juisi ya maembe
- Maembe yaliyo kaushwa
- Vikapu
- Jibini.

**Wauzaji wa pembejeo** ▶ **Wazalishaji** ▶ **Wasindikaji** ▶ **Wanunuzi na wauzaji** ▶ **Watumizi wa mwisho**

**Wauzaji wa pembejeo**
- Mafunzo
- Mbegu
- Ardhi
- Maji
- Vifaa vya hila

**Wazalishaji**
- Kupalilia
- Kunyunyizia maji
- Kutia vitambaa rangi
- Kukuasanya matunda/ maziwa
- Usindikaji wa mianzi ya kufuma vikapu

**Wasindikaji**
- Wakaushaji chakula
- Uzalishaji wa juisi
- Usindikaji wa kahawa
- Kutegeneza jibini
- Kuchoma nyama
- Kufuma vikapu

**Wanunuzi na wauzaji**
- Kuuza kwa soko la mtaa au kitaifa
- Maduka ya kijumla
- Matangazo
- Kufungafunga kwa kiasi tofauti

**Watumizi wa mwisho**
- Kitaifa
- Kimataifa
- Soko la ndani

Usindikaji wa mafuta ulifanyiwa wilayani lira,Uganda na maziwa yakauzwa katika mji wa Kampala. Ni jambo la muhimu kuelewa mahali pa kuuza bidhaa katika mzunguko wa thamani ili watu waweze kuamua ambapo hatua ya pili itatokea, wakati bidhaa zinasafirishwa ama zitafaa kwa mnunuzi au msindikaji.

Katika kila hatua kunaweza kuwa na sheria au kanuni kuhusu uzalishaji wa chakula, usindikaji, usalama na uuzaji wa bidhaa. Sheria hizi zinaweza kutambulika kupitia maswali yaliyo katika sehemu ya sera, taasisi na michakato.

### Mawazo ya kuboresha uzalishaji wa kilimo

Kwa watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi na pamoja na familia zao, ni muhimu sana kuboresha uzalishaji wa chakula na kuhakikisha wamepata lishe bora. Kuboreshwa kwa lishe bora kawaida hupatikana kwa kuongeza uzalishaji wa mboga na matunda. Kwa mfano, Kunde, kanga, mbaazi, maharagwe,na bidhaa za wanyama kama vile maziwa, mayai na nyama.

Vili vile ni muhimu sana kuboresha udongo. Chakula kinaweza kukua na kuongezeka wakati udongo ukihifadhiwa vizuri. Katika maeneo yaliyo na ukame, ni vuzuri kupanda mimea inayohimili ukame. Pia kukuza mimea mbalimbali ama kufuga kuku, nyuki n.k. Katika sehemu zilizo na mvua chache, ni vizuri kutayarisha mashamba mapema ili kupanda kwa wakati ufaao. Hili litahakikisha mavuno mema.

Kwa familia hohehahe zilizoathiriwa na virusi vya Ukimwi, ukosefu wa kazi unaweza kuleta wasiwasi sana. Hata hivyo, kama familia zinaweza leta rasilimali zao pamoja, wanaweza kusaidiana kudumisha uzalishaji.

**ZOEZI**

## Uchambuzi wa mzunguko wa thamani


Fanya mjadala kuhusu orodha ya bidhaa, mali na huduma zinazozalishwa na kikundi ulichokilenga.Kwa mfano, Kahawa, bidhaa za maziwa, mahindi, shanga, ususi wa nywele, sungura au papai n.k. Ziandike kwenye chati.

Je, kuna mahitaji mengi ya bidhaa au huduma hiyo? Piga mviringo bidhaa zinazohitajika sana sokoni. Sasa chagua tatu zilizo tofauti ili ziwakilishe zingine. (Unaweza pendekeza kugawanya bidhaa na huduma hizi katika vikundi vitatu.)

Katika chati, chora watendaji katika mzunguko wa thamani, kama ilivyo katika mzunguko wa kahawa, wauzaji wa pembejeo, wakulima, wauzaji, wanunuzi na watumiaji wa mwisho.

Sasa waweza kuamua kama thamani inaweza kuongezwa kwa bidhaa au huduma kwa kujibu maswali yafuatayo:

- Je, kaya zaweza kuongeza uzalishaji wao?
- Thamani yaweza kuongezwa kwa usindikaji zaidi?
- Bei ya soko inatofautiana na msimu? Kama ni hivyo, kuna uwezekano wa kuhifadhi bidhaa na kuiuza baadaye wakati bei zikiwa juu?
- Je, bei zinatofautiana na eneo la soko? Tunaweza kupata masoko mengine ?
- Ni nani anayeweza kusaidia kwa ushauri na kutoa uhusiano mpya na soko? Je, kuna mashirika yasiyo ya kiserikali , au watu wanaowakilisha kampuni wanaoweza kusaidia kuleta uhusiano huu?



Kama kuna majibu mazuri katika mojawapo ya maswali haya, basi kuna uwezekano wa kutumia uchambuzi wa mzunguko wa thamani ili kuongeza uzalishaji au faida. Tambua watu wanaoweza kusaidia kupata uchambuzi wa mzunguko wa thamani kwa undani zaidi. Kama kikundi undeni mpango wa utekelezaji.

**KIDOKEZO:** Zoezi hili si la kina katika uchambuzi wa soko. Lengo lake ni kuongeza ufahamu wa hatua tofauti za mzunguko wa thamani na kuhamasisha kaya zilizounganishwa na wafanyakazi wa ugani, mashirika yasiyo ya kiserikali na mashirika mengineyo yanayoweza kusaidia kwa kina.



*(Picha: Andrew Comings / Creative Commons Attribution Licence)*

## Mzunguko wa thamani ya ndizi nchini Kenya


Katika wilaya ya Thika nchini Kenya, kuna wakulima wengi wa ndizi. Ndizi zenyewe hutumiwa nyumbani na kuuzwa sokoni. Bei yake huwa ndogo na mahitaji ya kiasi kidogo. Uchambuzi wa mzunguko wa thamani ulifanywa na wakulima kwa kusaidiwa na wakala wa ugani.

Walitambua wauzaji wa kati wanao nunua kutoka kwa wakulima na kuuza katika maduka ya jumla mtaani Nairobi. Wakulima hawa walitambua kuwa kuungana na kuanzisha chama cha ushirika, wangekuwa na faida zao.

Wangepata mbolea na dawa kwa bei nafuu.Pia, wangeweza kukodisha lori kila juma la kusafirisha ndizi zao mjini Nairobi na kuziuza kule. Katika duka za jumla au sokoni.

Kama uzalishaji wa shirika la ndizi ungekuwa kwa kasi nzuri, kungekuwa na uwezo wa kuungana moja kwa moja na wanaouza bidhaa hii katika mji wa Nairobi au kwa wauzaji wanaosafirisha bidhaa katika soko la kimataifa.

**Jinsi mfumo wa soko la ndizi unavyofanya kazi nchini Kenya**



MASWALI YA MWONGOZO

# 5 Mzunguko wa thamani

Maswali haya yameundwa ili kuwasaidia washiriki kuchagua bidhaa zinazoweza kutumiwa katika mzunguko wa thamani, kubaini wahusika wengine (Wafanyakazi wa kilimo ugani, wafanyakazi wa serikali , mashirika yasiyo ya serikali na kampuni nyingine) ambao wanaweza kusaidia washiriki kufanya uchambuzi wa mzunguko wa thamani ili washiriki waongeze thamani katika bidhaa zao.

Wakati washiriki wakijibu maswali andika majibu yao kwa chati na ujaze nakala za **Maswali ya Mwongozo ya Sehemu ya 5** yaliyo katika ukurasa 46. Majibu hayo yanaweza kuachiwa kikundi na jedwali zikawekwa na anayeongoza. Hii itasaidia kufuatilia majibu yatakayotuongoza baadaye katika mchakato huu wa lenzi.

## 5a Ni bidhaa na huduma zipi zinazofaidika na uchambuzi wa mzunguko wa thamani?

Angalia katika huduma na bidhaa zilizo katika mzunguko wa thamani katika ukurasa 43 na pia katika zoezi la uchoraji wa ramani.

## 5b Ni nafasi zipi zilizopo kwa wazalishaji kuongeza thamani?

Baini mambo yanayoweza kuboresha thamani kwa washiriki. Kwa mfano Usindikaji wa bidhaa, uhusiano wa moja kwa moja na masoko, kuhifadhi na kuuza moja kwa moja na wateja.

## 5c Je, ni taasisi au mashirika yapi ambayo yanaweza kusaidia kufanya uchambuzi wa thamani katika jamii unazolenga?

Zingatia kuhusu yale mashirika uliyoyatambua katika uchambuzi wa mzunguko wa thamani ambayo yanaweza kusaidia.Je, kuna mengine?

## 5d Ni hatua gani zinazohitajika kuchukuliwa ili kuwasaidia wazalishaji au wasindikaji kuongeza thamani ya bidhaa zao?

Tambua baadhiya vitendo vya kuwahusisha waliobainika katika sehemu ya 5c ili wahusika waweze kuendelea mbele katika kuboresha thamani za bidhaa na huduma.



*Kuchambua mzunguko wa thamani kunaweza kusaidia kuongeza faida inayopatikana. (Picha: Moses Kamau Wanjiru / Samaritan's Purse)*

MASWALI YA MWONGOZO YA SEHEMU YA 5

# Mzunguko wa thamani

| **5a** Ni bidhaa gani na huduma zinaweza faidika kutokana na Uchambuzi wa mzunguko wa thamani? | **5b** Ni uwezekano upi (opportunities) uliopo kwa wazalishaji kuongeza thamani? | **5c** Ni taasisi zipi au mashirika katika jamii yanaweza kusaidia kundi unalolenga kutekeleza Uchambuzi wa mzunguko wa thamani? | **5d** Ni hatua gani zinahitajika kuwezesha wazalishaji au wasindikaji kuongeza thamani katika bidhaa zao |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |

SOMO LA SITA

# 6 Mikakati ya maisha

Mchanganyiko wa mali na shughuli ambazo familia huchagua mara nyingi hujulikana kama mikakati ya riziki. Hili ni chaguo ambalo watu hufanya ili kukidhi mahitaji yao na ustawi wa maisha yao siku za baadaye.

Mkakati wa riziki si shughuli tu za kuzalisha mapato bali ni pamoja na machaguo mengine ambayo watu hufanya. Hizi ni pamoja na ubadilishaji wa bidhaa au kazi ama kupunguza gharama ya matumizi ya nyumbani kwa kuwa na bustani ndogo ya mboga.

Pata wahusika wachangie baadhi ya mikakati ya riziki ambayo hufanya kazi vizuri na jamii yao.

### Mifano ya kawaida ya mikakati ya riziki

- Kurekebisha magari katika karakana
- Kutengeneza na kuuza pombe
- Kupanda mimea katika bustani ya nyumbani
- Mjakazi wa nyumbani
- Dereva wa lori la shirika
- Kuchunga magari
- Uhamiaji wa msimu kwa kazi
- Kuuza maua
- Kupanda miti ya matunda
- Kusindika chakula

### Mchanganyiko wa riziki

Ni muhimu kwa familia kuwa na mchanganyiko wa riziki ili kuhamasisha uendelevu. Kwa mfano, Baba anaweza kuwa dereva aliye na mshahara, mama awe na kijishamba cha nyumbani (kinachopunguza gharama ya chakula) dada anakausha na kuuza maembe wakati ndugu akihusika katika uvunaji na kupanda kwa jumuiya. Kila mtu anachangia kwa njia tofauti kwa manufaa ya kusaidia familia.

Waulize washiriki kufikiria kuhusu familia ambayo inajimudu. Tambua mikakati mbali mbali ya familia hii. Je, ni nani anayehusika kuhakikisha familia inajimudu?

ZOEZI

## Kuota ndoto




*Pengine ndoto yako ni kutengeneza nyumba nzuri ya jamii yako. (Picha: Jimmy Francis Odongo / Samaritan's Purse)*

Waulize washiriki wote kufikiri juu ya maisha ya usoni. Je, wanajiona wapi katika miaka mitano ijayo? Watataka kuwa na maisha yaliyobadilika vipi? Wangependa kufanya nini? Wanataka kuhusika na riziki gani? Wape wahusika muda wa kutosha ili wawaze na waote ndoto zao.Waambie kuwa ndoto zao zinastahili kuwa makinifu ipasavyo. Wahimize wafikiri kwanza juu ya uwezo wao wa (kujiamini, ujuzi, uwezo wa kufanya kazi kwa bidii, elimu) au nafasi zao(usaidizi wa serikali, uwezekano wa biashara ndogo ndogo, mafunzo ya mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na kadhalika, ili ndoto zao zitokane na misingi ya ukweli)

Waonyeshe mchoro ulio katika ukurasa 48. Waulize wachore, wawakilishe au waandike ndoto zao katika Kisanduku, kulia hapo juu, kisha wachore au wawakilishe mahala walipo sasa katika Kisanduku kushoto hapo chini. Waulize wahusika waweke michoro hii vizuri kwa ajili ya matumizi katika Sehemu ya 7.

**Kuota ndoto ya maisha mazuri ya siku za usoni…**



ZOEZI

## Ramani za riziki ya jamii

Kwa chati au mchangani, chora ramani kubwa ya jamii. Patia washiriki karatasi ndogo iliyo na gundi na uwaambie waandike riziki zao za sasa. Wekelea karatasi zile kwenye ramani pahali ambapo shughuli zao hufanyika. Sasa wapatie washiriki karatasi za rangi tofauti. Waulize waandike shughuli zinazofanywa na jamii zingine zinazojimudu. Hizi zinaweza kuwa ni pamoja na wachuuzi wa mitaani, wasusi, dereva wa teksi, mfanyikazi wa afisi au anayekuza njugu karanga. Kama awali, wekelea karatasi hizi katika sehemu walipo kwenye ramani.

Je, kwanini watu hawa wengine wanajimudu? Je, watu wanaweza kufikiria jinsi wanavyofanya ili ufanikiwa katika riziki zao?Kwa nini tunafahamu kwamba wanafanikiwa? Je, sisi hupima mafanikio kivipi?

Tia alama (Msalaba ua asteriki) kwenye kwenye riziki ambazo washiriki wangependa kufanya wenyewe.

*"Wale waliokuwa wakikaa bure, sasa wanajimudu. Kila mmoja wa Wanawake katika kikundi chetu sasa wanafanya kazi."*

Aliyefaidika na mafundisho haya







*Usafishaji wa viatu ni moja ya riziki mingi ambazo hazihitaji vifaa vingi vya bei kali. (Picha: Debora Randall / Samaritan's Purse)*

ZOEZI


# Kunyoosha mawazo yetu

Kwa kweli, inaweza ikawa msaada sana kwetu tukitumia akili zetu tunapowaza mbinu mpya za kujipatia riziki. Hapa kuna zoezi rahisi la kuonyesha uwezo wa utatuzi ambao si dhahiri mara kwa mara. Wape wahusika wote karatasi (Yaweza ikawa imetumika na unairejelea) waombe watafakari wanachoweza kufanya na karatasi ile. Waulize mawazo yao. Watu wanaweza kupendekeza kuwasha moto, kuuza kama karatasi chakavu. Toa changamoto kwa watu ili waweze kutafuta njia bora ya uzalishaji kutumia karatasi ile. Je, wanaweza kuitumia kutengeneza mduara mkubwa unaoweza kuwatoshea watu kumi au zaidi ndani?




Baadhi ya watu wanaweza tu kuchora mduara mkubwa ulio na picha za watu ndani, wengine huenda wakatengeneza boti za karatasi, mifuko na kadhalika. Jibu sahihi limeonyeshwa hapa chini.

Kunja karatasi ile mara mbili kisha ukate mistari inayounganika kwa makini. Kwenye mkunjo, mistari ile inabomolewa kwa uangalifu. Ukifanya hivi katika mistari laini, kuna uwezekano kwamba angalau watu kumi au zaidi huenda wakatoshea au wakapita kwenye mduara ule.




**FUNZO MUHIMU:**
**Anza na ulichonacho, hata kama ni Kidogo**

*"Mafunzo haya yamenifumbua macho. Sasa naweza kuona na kuelewa fursa zinazonizunguka!"*

Aliyefaidika na mafunzo haya ya Lenzi ya riziki

## Baadhi ya mikakati ya biashara ndogo ndogo za kilimo

**MIMEA ISIYO YA KAWAIDA** Mimea maalum k.v. uyoga au mimea ingine ambayo yaweza kusagwa au kukamuliwa ili kuongeza thamani, kukoboa karanga, kuzalisha mafuta kutoka kwa alizeti (sunflower) yapaswa kuzingatiwa.

**MABWAWA YA SAMAKI** Mahali ambapo kuna uhakika wa kupatikana kwa maji, kuanzisha mabwawa ya samaki huleta mapato mazuri na lishe bora. Ufugaji wa samaki ni njia bora ya kutumiai viporo vya chakula jikoni, mbolea ya mifugo, matawi ya mimea na kwekwe (Weeds) kuwa madini ya protini ya hali ya juu na yanayoweza kusagika kwa urahisi.

**BUSTANI ZA NYUMBANI** Upanzi wa miti ya matunda au miti ya koko (Nut) karibu na makazi inawezekana. Hii ni njia bora pia ya kutumia maji taka kutoka nyumbani. Miti k.v. parachichi (Avocado) korosho (Cashew nuts) na miembe huenda yakatoa mazao mazuri ya chakula na mapato yakifedha kwa kutumia ajira chache.

**UKULIMA WA SHAMBA NDOGO NYUMBANI** Hii inamaanisha bustani au shamba ndogo karibu na makazi bora kwa ajili ya mboga na mimea ya miti shamba. Inasaidia katika lishe ya familia, ni rahisi kushughulikia hata kwa mtu ambaye huenda anaugua.

MASWALI YA MWONGOZO

# 6 Mikakati ya maisha

Utaratibu huu utawasaidia washiriki kuchambua hali zao kwa kuzingatia mikakati yao ya kujikimu maishani pia kuanza kutambua na kuzipa umuhimu suluhisho zao. Pia itakusaidia kuzielewa hali zao zaidi ili uweze kuwasaidia katika mahitaji yao.

Kama awali, rekodi majibu ya washiriki na ujaze katika nakala ya **Maswali ya Mwongozo ya Sehemu ya 6** ukurasa 52. Nakala hii iwekwe na mwezeshaji kwa ajili ya matumizi katika sehemu ya mwisho.

## 6a

**Je, sasa washiriki wana riziki gani?**

Rejea ramani ya jamii ya awali.

## 6b

**Je, ni riziki gani inayoonekana kuwa imefanikiwa katika jamii yako? (Rejea ramani ya jamii)**

- Waza kuhusu watu katika jamii wanaoishi katika nyumba za matofali. Je, wana kipato aina gani?
- Waza kuhusu watu katika jamii wanaopeleka watoto wao shuleni. Je, riziki yao ni zipi?
- Waza kuhusu watu katika jamii wanaokula vizuri. Je, kipato chao ni kipi?

## 6c

**Tafakari sasa kama riziki hizi zinaweza kuongeza hatari na kufanya maisha kuwa magumu kwa kipindi kifupi au kirefu kijacho. Kwa mfano. Je, zinaweza kuweka familia katika hatari ya kuambukizwa Virusi vya ukimwi? Ama katika hatari inayotokana na vita au uhalifu? Tumia rangi nyekundu kupiga mduara katika hatari hizi.**

## 6d

**Rejea zoezi la kuota ndoto: Je, washiriki wanatamani kuwa na riziki gani? Piga mduara ukitumia rangi ya samawati. Nini kinachowazuia kufuata riziki hizi?**

Angalia mikakati ya mapato iliyoainishwa katika 6b. Je, washiriki wanawaza jinsi watatimiza ndoto hizi? Karibu na kila mikakati iliyokatika ramani, andika mambo ambayo yanawasitisha watu kufikia riziki ya ndoto zao. Inaweza kuwa ukosefu wa ujuzi, fedha za kuanzisha biashara, ardhi au vifaa.

**KIDOKEZO:** Ni muhimu kutambua ndoto za watu lakini ni muhimu zaidi kuangalia kama wana mali na uhakika wa kuwawezesha kuendelea. Unaweza kuuliza watu warejee rasilimali zao na wajiulize kama mali hizo zitawawezesha kufikia ndoto zao kwa muda mfupi au muda mrefu. Watu wanaweza kuwaza kuhusu mikakati ambayo itakuwa ngumu kwa watu wanaoishi na Virusi vya ukimwi (VVU).

## 6e

**Ni hatua gani zinahitajika ili watu washiriki riziki hizi? Je, waweza kufanya nini ili kupunguza hatari zilizotambuliwa katika 6c?**

Hili ni swali muhimu sana. Tambua hatua kulingana na mapungufu yanayobainishwa katika 6d. Watu wanahitaji kujikumbusha kuhusu rasilimali walizonazo na zilizoko katika jamii yao. Inafaa watafakari kuhusu mzunguko wa thamani na njia bora ya kupata kushiriki katika riziki wanazozitamani. Je, kunazo sera, taasisi na michakato zinazotoa ushauri, msaada au mafunzo? Wanahitaji kutafakari juu ya hatari yoyote inayohusika na jinsi inaweza kupunguzwa.

MASWALI YA MWONGOZO SEHEMU YA 6

# Mikakati ya riziki

| **6a** Je, wahusika wana jihusisha na riziki gani sasa? | **6b** Ni riziki gani zimejimudu zaidi katika jamii? | **6c** Je, ni jinsi gani riziki hizi zinaweza kuongeza hatari au athari? | **6d** Je, wahusika wana ndoto kuhusu riziki zipi ambazo wangependa? Ni nini kinachowazuia kuzifuata riziki hizi? | **6e** Ni hatua gani zinahitajika ili wahusika wajihusishe na riziki hizi? |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

SOMO LA SABA

# 7 Kuchukua hatua



*Kufuga sungura ni njia muhimu ya kusaidia familia kupata nyama au mapato. (Picha: Moses Kamau Wanjiru / Samaritan's Purse)*

Sehemu hii ya mwisho husaidia kuleta pamoja taarifa zote zilizokusanywa kabla ya kuzipa kipau mbele na kutenda lolote. Sehemu hii inawawezesha washiriki kuunganisha majibu na mapendekezo yao kama matokeo ya kutumia lenzi ya riziki katika maeneo mbalimbali yanayozingatia rasilimali. Mazingira magumu na hali ya kukabiliana, sera, taasisi, na michakato, pamoja na mzunguko wa thamani na mikakati ya riziki.

Ujumbe huu utawasaidia kuyapa kipaumbele mapendekezo na ufumbizi wa kutekeleza mikakati. Ujumbe huu pia utawasaidia kuanza kupa vipau mbele kwa mapendekezo au suluhisho. Mbadala yakuishi,ujumbe huu utawasaidia wahusika na wawezeshaji kuelewa vipau mbele vyao na aina ya msaada wanaohitaji ili kufanikiwa.

Kwa kufuata sehemu za awali za lenzi hii ya riziki, washiriki wataweza kubuni mikakati zifaazo kwa maswali yafuatayo:

**2d** **Hatua za kuboresha matumizi ya au uwezo wa kupata raslimali.**

**3d** **Hatua za kuhimiza mikakati mizuri ya kukabiliana**

**4e** **Hatua za kushawishi au kuhimiza uwiano wa sera, taasisi na michakato inayohusika.**

**5d** **Hatua za kuwezesha watu kusonga mbele katika mzunguko wa thamani.**

**6e** **Hatua za kuwezesha watu kushiriki katika riziki mbadala.**

Hatua hizi zote zimeandikwa katika safu ya mwisho ya chati katika kila hatima ya sehemu hizi tano. (Kama chati hizo hazikutumiwa, kusanya hatua zilizo pendekezwa katika mwisho wa kila sehemu ya mafunzo) Kwa pamoja hatua hizi zitawakilisha mapendekezo chanya ambayo yamebuniwa wakati wa mafunzo ya lenzi ya riziki. Kwa sababu wahusika huchukua miezi kadhaa kabla ya kuhitimu mafunzo ya lenzi ya riziki, hatua hizi zitatoa kumbukumbu nzuri kwa mafunzo na vitendo vilivyokubaliwa.

*"Hapo mwanzo, sikudhania kuwa watendaji wa serikali za mitaa ni rasilimali, lakini sasa nina jiamini katika kuingia afisi yoyote na kuomba ushauri au msaada."*

Aliyefaidika na mafundisho haya

# Kuipa umuhimu shughuli ya hali ya maisha

Kukubali ni shughuli zipi za riziki zinazoweza kuchaguliwa na kufuatiliwa kunaweza kuwa na changamoto sana. Kutakuwa na shughuli za riziki ambazo vikundi vitajiingiza kwa pamoja au kibinafsi. Katika sehemu hii, Zingatia shughuli za pamoja, lakini kama kuna nafasi, himiza watu binafsi kubuni chaguzi zao wenyewe (binafsi au kama familia) kufuatia mchakato huo huo. Unaweza kuwa na mkutano mwingine wa kutoa muda zaidi ili kusaidia watu katika shughuli hii. Vinginevyo, fanya mpango wa kutembelea kila mshiriki kivyake baada ya mkutano.

Huenda mchakato huu ukachukua mikutano kadhaa baina ya shirika au kanisa linalowezesha shughuli hii zima, ili kuona jinsi gani wanaweza kutoa msaada kwa wanachama wa kundi lengwa

## Msaada wa nje

Shughuli nyingi zilizobainishwa zinaweza kufanywa bila msaada wowote wa nje. Hii ni baadhi ya sababu ya kutumia lenzi ya riziki/ maisha. Ni kusisitiza kwamba hata maskini wanaoishi katika mazingira magumu wana mali, chaguzi na mikakati ya kujitambulia.Hali ya kuwa na wakati kwa vikundi na kuchambua hali katika kioo cha maisha inaweza kuchukua hatua hata bila ya msaada. Hata hivyo vikundi vinaweza kuhitaji msaada wa nje. K.m kutoka kwa kanisa la kwao au asasi zisizo za kiserikali. Katika hali nyingi inaweza kuwa suala la kujenga uhusiano au msaada kutoka kwa wadau wengine ili kundi lako linufaike na huduma zao.

## Vigezo vya uteuzi

Kanuni za kuzingatia wakati wa kuchagua hatua za kuingilia kati za riziki zitakazosaidiwa ni pamoja na:

**ENDELEZA KWA KILICHOPO** Shughulikia na kusaidia majibu chanya yaliyopo tayari na utumie rasilimali (ambazo hazitumiki kikamilifu) kila inapowezekana. Jamii, familia za mbali na familia zima zina njia zao za kukabiliana na migogoro.

Njia mpya za kukabiliana zinaweza kubuniwa ili kukabiliana na migogoro na hatari mbalimbali. (pamoja na athari za virusi vya ukimwi) japo jamii zingine na familia zitachukua muda kukubali kabisa. Mara nyingi itakuwa nafuu kuigharamia uendelevu na kuimarisha mikakati iliyopo.

**USIFANYE MADHARA** Hakikisha washiriki wametafakari madhara yoyote yanayoweza kutokea kutokana na njia walizopendekeza za utekelezaji. Kwa mfano, Je, inawezekana kwamba kwa kuboresha njia za kufika mjini au sokoni kutaongeza hatari za kuambukizwa virusi vya ukimwi kwa wanafamilia? Ama kwa kuhamasisha vijana kujiunga na kituo cha msaada, wasichana wanaweza kuwa katika hatari fulani iwapo hawasimamiwi? Vile vile, je, kwa kuhimiza wajane kutetea haki zao katika familia walionyakua mali zao (baada ya wame zao kuaga) familia zinaweza kuwadhibu wajane mara tu wanapoanza kutetea haki zao?

Tambua vyanzo vyote vya madhara iwezekanavyo kisha ufikirie njia muhimu za kuondoa madhara haya.

**LENGA UENDELEVU** Himiza washiriki wachukue maono ya kudumu kuhusu mali, pembejeo, raslimali na soko tarajiwa.



*Wasilisha vyakula kwa njia inayovutia kwa wateja. (Picha: Moses Kamau Wanjiru / Samaritan's Purse)*

Kuchagua mikakati ya riziki ambayo itakidhi mahitaji ya muda mfupi inahitaji jitihada na mabadiliko katika siku zijazo. Kusema ukweli mikakati sahihi ya riziki itakuwa na uendelevu katika njia zote – ikiwa ni pamoja na malighafi na pembejeo zinazohitajika. (Kwa mfano, Je, malighafi itapatikana kwa muda mrefu?) mahitaji ya kufanya kazi. (Je, udhoofu wa afya utakuwa na athari gani?) na mahitaji ya soko. Kwa mfano, Kila familia inahitaji chujio moja ya maji ilhali riziki zinazohusu ugawaji wa chakula ama ususi wa nywele zitakuwa na hitaji ya endelevu.)

**ZOEZI**

## Matunda yanayoning'inia

Chora mchoro wa mti katika chati. Andika shughuli zote zinazopendekezwa kama miduara midogo (Maumbo ya matunda) Angazia kila tunda (shughuli) moja kwa moja bila mpangilio wowote. Jadili pembejeo zipi zinahitajika kufanikisha kila shughuli. Kama shughuli hizi zinawezakufanywa na washiriki bila usaidizi wa nje, chora tunda hili ukitumia rangi nyekundu. Kama (Tunda) shughuli itahitaji msaada wa kijiji, pengine kutoka kwa kanisa au jumuiya ya mashirika, tumia rangi ya samawati kwenye tunda hili.Kama shughuli itahitaji msaada wa nje, mafunzo au ufadhili ambao haupatikani kwa kikundi kwa urahisi kupitia kwa mashirika yaliopo au huduma zilizo katika jamii, chora (Tunda) ukitumia rangi nyeusi.

Zoezi hili litapendeza sana likifanyika mchangani au ukitumia karatasi kubwa, kwa sababu wahusika watatembea tembea.




Kwa kutumia gundi, bandika matunda kwenye mti. Kwa matunda ambayo mshirika ataona rahisi kwao kufikia, yabandike karibu sana (Mahali yatakayofikiwa kwa uepesi) kwa ujumla,mengineyo yatakuwa ni yale matunda mekundu ilhali matunda ya samawati na yale meusi yataweza kuwa na ugumu kidogo kufikia. Hakikisha kila mshiriki ameona na kupendezwa na msimamo wa tunda kwa mti huo.

Sasa jadilini kila tunda / shughuli ilioning'inia chini zaidi katika mti. Amueni ni kiongozi yupi atakaye hakikisha shughuli hiyo imefanywa. Baadhi ya kazi zitakuwa rahisi na zinaweza fanywa na mtu mmoja. Zingine zitakuwa ngumu na zitahitaji mkutano mwingine katika kundi. Kwa hivyo, ni jambo la muhimu sana kupata mtu mmoja awe na jukumu la kuongoza kikundi na kufuatilia kila shughuli.

MUHTASARI WA PAMOJA WA SEHEMU YA 7

# Kuchukua hatua

| **2d** Hatua za kuboresha matumizi ya, au ufikishaji wa rasilimali | **3d** Hatua za kuimarisha mikakati mingi chanya | **4e** Hatua za kushawishi sera, taasisi na michakato halisi. | **5d** Hatua za kuwawezesha wahusika kusonga mbele katika mzunguko wa thamani | **6e** Hatua za kuwezesha wahusika kujihusisha na riziki mbadala na kupunguza hatari | **Vipau mbele vya Matendo** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |

ZOEZI

## Kubuni hatua za hali ya maisha ya kikundi

Zoezi hili la kupanga litasaidia washiriki kuangazia vitendo vyote ambavyo wamevitambua na kuupa umuhimu ufumbuzi. Pia litasaidia kutambua ufumbuzi wanaoweza kupata wenyewe na ule wanahitaji usaidizi kutoka kwa kanisa, jamii au mahali pengine.

- Katika kikundi, rejeeni nakala iliyokatika ukurasa 56 ambayo inawezesha washiriki kuleta pamoja safu zote za mwisho zikionyesha vitendo viwezekanavyo kutokana na lenzi ya riziki.
- Sasa imarisha mawazo haya katika safu ya mwisho huku ukibainisha na kuondoa marudio yote. Hatimaye, unastahili kuwa na safu ya mwisho inayoorodhesha shughuli zote zilizo orodheshwa. Hesabu mawazo ambayo yametokea mara kadhaa.

ZOEZI

## Kuorodhesha katika jozi

Zoezi hili litahitajika tu kama watu wanapata ugumu kukubaliana ni shughuli gani itakayopewa kipau mbele. Kama kuna chaguzi tatu au mbili tu, basi zoezi hili si la lazima. Kwa mfano zoezi rahisi la kuorodhesha vyeo kwa kutumia maharage ili kupigia kura shughuli mbalimbali, la weza tosha.

Hata hivyo zoezi hili ni muhimu sana kama chaguzi zimekaribiana sana na iwapo kuna shughuli nane hadi saba za kuzingatia.



*Waliofaidika kutokana na mafundisho ya lenzi ya riziki hupata kujiamini na uwezo wa kutumia rasilimali zao. (Picha: Moses Kamau Wanjiru / Samaritan's Purse)*

- Andika kila shughuli katika kadi mbili tofauti. Gawa kadi hizi katika seti mbili za kufanana. (kwa kadi zinazofuatana). Chora jedwali katika chati lililo na safu / mistari mingi zaidi kuliko idadi ya kadi. Kama shughuli ni saba, jedwali liwe na safu nane.
- Bandika seti moja ya kadi katika mistari kutoka juu hadi chini na kadi isiyoandikwa sehemu ya juu.
- Sasa weka seti nyingine katika mstari kotoka kushoto kuelekea kulia. Karibu na kadi ambayo haijaandikwa (Angalia mchoro.)
- Kwa miraba iliyo na chaguzi za kufanana, hakikisha umeziacha hivyo bila chochote. Vivyo hivyo na kwa jozi zilizorudiwa katika kona ya chini ya kulia.(Kama ilivyo katika picha)
- Sasa linganisha chaguo la kwanza lililo sehemu ya juu kushoto na chaguo la kwanza la mstari wa juu. Himiza washiriki wajadiliane ni chaguo lipi watakalolichagua. Chora ama andika chaguo hili kwenye safu.
- Sasa endelea na mchakato huo huo kwanzia safu ya kushoto ukielekea kulia. Halafu endelea hivyo hivyo mpaka chaguo zote zimelinganishwa.
- Vijisanduku vyote katika gridi ambavyo awali havikuwa vimechorwa vinapaswa kuwa vimejazwa. Hesabu idadi ya kila chaguo kama inavyotokea katika gridi. (Usihesabu kadi ya kwanza iliyo kwenye mstari wa juu na upande wa kushoto)
- Orodhesha chaguzi kwa mpangilio kulingana na idadi yao katika gridi. Chaguo lililochaguliwa mara nyingi litakuwa la kwanza kuorodheshwa.

**Kuorodhesha katika jozi – jedwali iliyokamilishwa**

| | Pata mafunzo ya ususi | Anzisha ufundi wa baiskeli | Endesha teksi | Kuuza sukari na chai | Kulisha sungura | Anzisha kikundi cha muziki |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Anzisha kikundi cha muziki | Pata mafunzo ya ususi | Anzisha ufundi wa baiskeli | Endesha teksi | Kuuza sukari na chai | Anzisha kikundi cha muziki | |
| Kulisha sungura | Kulisha sungura | Kulisha sungura | Endesha teksi | Kulisha sungura | | |
| Kuuza sukari na chai | Pata mafunzo ya msusi | Anzisha ufundi wa baisikeli | Kuuza sukari na chai | | | |
| Anzisha ufundi wa baisikeli | Pata mafunzo ya ususi | Anzisha ufundi wa baisikeli | | | | |
| Anzisha ufundi wa baisikeli | Anzisha ufundi wa baisikeli | | | | | |
| Pata mafunzo ya ususi | | | | | | |

Washiriki sasa wanaweza kupunguza orodha kwa chaguzi tatu au nne (kwa kuzingatia vipau mbele) ambavyo wataingiza kama mikakati ya riziki inayohitaji pembejeo za nje.

Kama awali chagueni mtu atakayechukua jukumu la kuongoza shughuli za samawati na nyeusi. Tunda/ shughuli. Kama zilivyochaguliwa

# Mipango ya kuchukua hatua

Pitia kila shughuli iliyochaguliwa na ubuni mpango wa utekelezaji. Anza na shughuli ambazo watu wanaweza kufanya bila msaada wa nje. Kwa shughuli zinginezo, hatua ya kwanza yaweza kuhusisha mkutano na shirika lisilo la kiserikali (NGO), Afisa wa mamlaka ya mtaa au taasisi zingine. Hii itawasaidia kuwasilisha matakwa ya kikundi na kuomba msaada.


Wanaweza kuamua kuomba msaada kwa mashirika zaidi ya moja kulingana na msaada ambao wanahitaji. Hata hivyo watu wanaweza kuendelea na shughuli ambazo watajifanyia wenyewe.

Buni mpango rahisi wa utekelezeji kuhakikisha kwamba shughuli zote ambazo zimepatiwa kipau mbele zitatekelezwa. Maswali yafuatayo ya vidole vitano ni mbinu saidizi katika kupanga mambo na katika kujibu maswali yote,na itapelekea kila shughuli ifanyike kwa ufanisi.



*Watu wanaomiliki duka na kuwajua wateja wao vyema na mambo au bidhaa wanazopendelea sana huwahimiza kurudi tena katika duka lile. (Picha: Moses Kamau Wanjiru / Samaritan's Purse)*

- **NINI** – je, ni shughuli au kazi gani unaipanga? Kwa nini inahitajika?
- **VIPI** – je, kazi hiyo itatekelezwa vipi? Ni rasilimali zipi zinahitajika?
- **NANI** – je, ni nani atatekeleza kazi hii? Watahitaji mafunzo?
- **WAPI** – je, kazi hii itafanyika wapi?
- **LINI** – je, kazi hii itafanyika lini? Itachukua muda gani?




## Vipe kipau mbele shughuli zilizochaguliwa na uunde mpango wa utekelezaji

| Ni shughuli gani itakayofanyika? | Shughuli itafanyika vipi? Ni rasilimali gani zitahitajika? | Ni nani aliye na jukumu la kutekeleza? | Je, kazi au shughuli itafanyikia wapi? | Lini? ipi tarehe stahiki? | Watu gani watakaofuatilia? |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. Anzisha vikundi vya kuweka akiba za familia. | Vitabu, mwalimu, kalamu, mtaala wa kufundishia. | Eva atashirikiana na shirika la Center for Urban Mission kupanga mafundisho na ataunda vikundi | Mafunzo na mikutano itafanyika katika jengo la kanisa na kumbi zingine zilizopangwa. | Aprili 24. Saa saba mchana hadi saa kumi jioni. | Idadi ya vikundi vilivyoundwa |
| 2. Mafunzo ya mbinu mpya za kilimo. | Mfanyakazi wa ogani, penye mashamba au mahali pa mafunzo, Mbegu, jembe | Juma apange pamoja na mfanyakazi wa ogani | Shamba la Juma | Mwisho wa Agosti Tarehe itakayo kubaliwa baada ya mkutano. | Idadi ya watu waliofundishwa na wanatumia mbinu mpya za kilimo |
| 3. Mradi wa kuku | Mbao, nyundo, misumari, lishe ya kuku,pipa la maji na chama cha ushirika. | Hamisi akutane na mfanyakazi wa ogani ili wapange siku za mafunzo | Katika ofisi ya shirika lisilo la kiserikali | Septemba | Idadi ya watu waliofundishwa waanzishe miradi mipya. |
| 4. Utetezi kwa viongozi wa kijiji kuhusu basari za shule kwa familia | Kutana na mamlaka ya kijiji kubaini kama familia zitapata basari | Fatuma na maria wakutane na kiongizi wa kijiji | Katika ofisi ya mkuu wa wilaya | Mei, 15 | Idadi ya familia zinazohitaji basari za shule |

# Kubuni mikakati ya riziki ya mtu binafsi

Rejea ramani ya kuota ndoto iliyo katika ukurasa 48. **Sehemu ya 6**. Katika sehemu ya kulia (A) kuna picha inayoonyesha mambo yote ambayo ungependa yatokee katika nyumba yako siku za usoni. Kwa hiari yako unaweza kurekebisha kidogo.

Kumbuka msingi wa ndoto zako ni hali uliyonayo sasa. Andika matarajio yako yote chini ya picha katika chati hiyo hiyo, upande wa kushoto uliyochora hali yako ya sasa (B). Andika chini ya picha hiyo jinsi unavyoona mambo yalivyo sasa. Je, kuna tofauti kubwa kati ya mambo ya sasa na matumaini ya ndoto yako ya baadaye? Je, kwa nini unataka mabadiliko?

Katika nafasi iliyo katika sehemu ya juu (C), orodhesha rasilimali zote ulizo nazo binafsi, mikakati ya kukabiliana nayo, shughuli za sasa na sera, taasisi na mchakato utakayotumika (PIPS) – vipengele vyote chanya vinavyohusiana na mbinu hii ya lenzi ya riziki zinazokupatia nafasi za kujiendeleza. Yaweke haya yote kwa msingi wa matokeo ya sehemu zote tano za lenzi hii ya riziki za hapo awali zinazohusiana nawe binafsi.

Katika nafasi iliyo hapo chini kulia (D), andika matatizo yote, vikwazo na mizigo inayositisha ndoto zako.

Katika kuungunisha sanduku A na B ni ngazi. Vipandio vilivyo katika ngazi zinawakilisha hatua ama mabadiliko yote ambayo yatafanywa ili kukusongesha karibu na kutimiza ndoto zako.

Sasa anza kuorodhesha shughuli (E) ambazo utahitaji ili uanze kupanda juu ya ngazi. Anza kwa mabadiliko rahisi. Tumia mishale kuelekeza nafasi zile muhimu utakazozifikia – au kuonyesha matatizo unayoyafahamu. Piga mduara katika pembejeo ambazo utazihitaji kama mufunzo, ushauri au mkopo.Kumbuka kuna vikwazo unavyohitaji kushinda.

Hakuna haja ya kukamilisha hatua zote kwa sasa. Anza kwa hatua chache za kwanza. Anza na zile ambazo unaweza kuzitimiza kwa urahisi. Baadaye unaweza rejea kwa chati hii ili utimize hatua zingine. Ongeza tarehe baada ya kila hatua kutimizwa.

*" Ninahitaji kujiamini kisha nitaweza kubadilisha hali niliomo pole pole"*

Aliyenufaika na mafunzo haya

## Kufanya mabadiliko

Robert alikuwa akiishi na virusi vya ukimwi lakini alikuwa akipata matibabu ya ARV. Alipata mafunzo ya lenzi ya riziki. Aliporudi nyumbani, alijiunga na mpango wa kuweka akiba. Baada ya mwaka wanachama wote waligawanya mapato (Pamoja na riba).

Robert alijadili mikakati na bibi yake. Walikubaliana kuajiri watu watengeneze matofali ambayo Robert alioka na kuuza. Baadaye, Robert aliajiri watu wakamjengea nyumba ya tofali.

"Nilipopimwa na kupatikana na virusi vya ukimwi, nilipatwa na shinikizo la akili na afya yangu iliendelea kudhoofika sana mpaka nikafikiri kwamba siku zangu zimeyoyoma sana." Robert alisema.

"Lakini nilipojiunga na jopo la kanisa nikawa nafundishwa, nilitiwa moyo sana. Tumaini hili limenisaidia sana na ninaamini nitafanya makuu maishani. Sasa familia yangu inaweza kujimudu na maisha lakini mwanzoni ilikuwa shida kujimudu kwa mahitaji ya msingi."

Sasa mbali na kikundi chake cha awali, wamebuni kikundi kingine cha pili kwa sababu watu wengi wanajiunga hasa wanapoona yale aliyafanya Robert. "Watu wengi wanaoishi na virusi vya ukimwi huona tu mauti mbele yao." Robert anasema. Lakini sasa amejenga nyumba ya kudumu na ameajiri watu wamsaidie kwa sababu ya hali yake ya afya. Ametumia mali yake ya udongo na kuigeuza kuwa matofali. Hali kadhalika, sasa anaonekana kuwa mtu aliye na thamani na unyanyapaa aliokumbana nao kutokana na hali yake ya kiafya umekwisha kabisa.

## C Nguvu na nafasi

- Bidii
- Mtandao mzuri wa marafiki
- Kundi la kuweka akiba
- Ushirika mzuri na kanisa
- Mafundisho yanayotolewa na mashirika yasiyo ya kiserikali
- Wingi wa maembe kutoka kwa shamba la familia



A

Kuishi katika nyumba nzuri

Kuwa na akiba

Lishe mara mbili au tattu kwa siku

Watoto wenye afya na wanaosoma

## E Shughuli

Kufungua duka la ususi wa nywele hapo nyumbani

Kununua makasi na vifaa

Kuhudhuria mafundisho ya jioni ya ususi wa nywele

Kupelekea watoto shuleni na kurekebisha nyumba

Kuuza maembe yaliokaushwa kupitia ushirika wa mtaa

Hudhuria mafundisho ya jinsi ya kukausha maembe

Kuwa mshiriki wa kundi la kuweka akiba



B

Uuzaji wa maembe kando kando ya barabara

Ukosefu wa karo ya shule

Nyumba inayovuja katika kitongoji duni

Lishe mara moja au mara mbili kwa siku

## D Matatizo, vikwazo na mizigo

- Ukosefu wa mapato ya kila siku
- Afya duni
- Ukosefu wa ujuzi
- Kutoweza kupata mkopo kutokana na ukosefu wa akiba ya kutosha
- Shinikizo la akili
- Ukosefu wa pesa za kutosha za chakula, karo au sare za shule kwa wanafunzi

SOMO LA NANE

# 8 Kuiga na kufuatilia



Ujuzi wa kujenga ni muhimu sana
(Picha: Debora Randall / Samaritan's Purse)

Jukumu la makanisa au la mashirika yanayotaka kutekeleza lenzi ya riziki inastahili kuwa katika kuhamasisha na kuongeza ufahamu (kwa kutumia mawazo yaliyotolewa katika **Sehemu ya 1** ukurasa 8) kwa kuchagua wanafunzi na kuwatia moyo wakati wa mafundisho. Pamoja na hayo, ni muhimu sana jarida hili litafsiriwe kwa lugha nyingi za mama kama iwezekanavyo.

Kuna mbinu kuu mbili za kutumia lenzi ya riziki. Mbinu ya kwanza ni ya moja kwa moja ambapo wawezeshaji hufanya kazi moja kwa moja na washiriki katika jamii. Mbinu ya pili ni ya uwezeshaji unaotoa uwezo, ambapo wawezeshaji hufunzwa halafu huenda kutumia lenzi hiyo na washiriki. Wawezeshaji hao wanaweza kuwa viongozi wa mtaa, washiriki wa kanisa au wanachama wa shirika fulani. Wakati mwingine mafunzo haya yatahitajika kurudiwa mpaka washiriki waelewe vizuri. Hakikisha kwamba wao wana ujasiri na usahihi wa kuwafundisha wenzao.

Kwa kutumia mbinu ya pili ya kuchagua wanafunzi kumbuka ni muhimu kuchagua mashirika zaidi ya moja na kuchagua washirika, kumbuka kwamba ni vyema kuchagua zaidi ya kikundi kimoja, kanisa au shirika.

Kwa mfano, kundi fulani la kujitegemea linaweza kuulizwa lichague wanachama wawili au watatu ili wapate mafunzo. Hii itahakikisha kwamba wanakamilisha mafunzo hata kama kutakuwa na tatizo kama ugonjwa fulani kwa familia. Halafu wao wanaweza kusaidiana katika kutekeleza mambo waliokubaliana. Kama mbinu ya uwezeshaji wa kujenga itatumika, inamaana kwamba mwanafunzi mmoja au zaidi anao ujasiri wa kuiga mafunzo hayo kwa wanachama wengine.

*"Sasa watu hawa wanaweza kupeana kanisani!"*

Mhubiri,
Korogocho
Nairobi

## Mabadiliko yaliyoonekana

Mafunzo ya lenzi ya riziki yalifanywa kwa walengwa wa makanisa kumi katika kijiji cha Korogocho, Nairobi. (Walichaguliwa kwa sababu walionekana kuwakatika mazingira magumu) walionekana wanajiheshimu na kujiamini sana. Kundi la watu wanaoweka akiba walitiwa moyo sana.

Vijana walitambua vipawa vyao.(kwa mfano uimbaji na uigizaji) kama mali ya thamani. Tangu wakati huo wa mafundisho, biashara kumi na mbili mpya zimeanzishwa. Watu watano kijijini Korogocho waliweza kufungua akaunti na kuanza biashara.

Wachungaji pia wameshuhudia mabadiliko "Walengwa si mzigo sasa kama walivyokuwa hapo awali, wakiwa omba omba na kutaka kuonewa huruma kila mara. Foleni kubwa za watu wanaohitaji msaada hazipo tena. Sasa watu wanapeana huduma na mali kanisani."

# Ufuatiliaji

Kwa mbinu hii ya lenzi ya riziki kufanikiwa, ni muhimu maelekezo ya kutosha kuhusu mchakato mzima yatolewa. Je, tutahakikishaje kuwa usahihi unakuwepo wakati mbinu ya pili inatumika?

Wawezeshaji wapya waliofunzwa watahitaji ufuatiliaji unaoendelea ili waweze kuwafundisha wengine. Wafanya kazi wa mashirika wanaweza kutoa msaada wa kufuatilia kila wakati watu wengine wanapofundishwa. Lakini ni muhimu wawasaidie wanaoongoza mafunzo – kuwahimiza na kuwajengea uwezo – bila kuchukua muda mwingi wakati wa mafunzo na kuathiri uwezo wao wa kujiamini. Vipengele vingine vya mwongozo huu ni vigumu sana kushirikisha. Kwa mfano, mafunzo ya Sera, taasisi na mchakato (PIPS) huwa na changamoto mingi sana na ni mada ambayo watu huenda wakafurahia msaada.

Watu wanahitaji kutekeleza lenzi hii wenyewe, au kuwasaidia wengine katika kutekeleza, kabla ya kupata ujasiri na uzoefu – pengine mara kadhaa. Kwa hiyo si kweli kutarajia watu wapya waliofunzwa kutwa mara moja. Mchakato wa ufuatiliaji unaweza ukahusisha mikutano ya kurejelea kwa miezi michache kwa kuangalia vipengele tofauti. Hili litawapa wanafunzi wapya nafasi ya kuuliza maswali na kupata usaidizi wa matatizo yoyote wanayokumbana nayo.

Baada ya mwaka mmoja au zaidi, wanafunzi hawa wapya watakuwa sawa.

# Pembejeo za mafunzo

Mafunzo haya ya lenzi hii ya riziki yanaweza yakatolewa kwa semina au warsha ya siku tano. Lakini ukweli ni kwamba, makundi machache ya kujitegemea (SHG), wanaojitolea au wanachama wachache wanaweza kupata siku tano mfululizo za mafunzo hata nyakati legevu katika mwaka. Aidha, kuna faida kubwa sana kupata muda wa ziada baada ya mafunzo ili wanafunzi waweze kubaini namna ya kutekeleza yale waliyofundishwa.

Katika maeneo ya mijini nchini Kenya, mafunzo yalitolewa kwa vikao vya siku moja vilivyodumu kwa miezi kadhaa. Katika maeneo ya shambani, nchini Uganda, mafunzo yaliendeshwa vizuri kwa kuanza vikao adhuhuri baada ya kazi za shamba za siku kukamilika.

Watu wazima hujifunza vyema sehemu kwa sehemu – katika vikao vifupi wala sio vikao virefu sana.

# Kufuatilia na kutathmini

Buni njia ambazo wanafunzi wataweza kufanya ufuatiliaji wao na kutoa maoni. Chati zilizo katika kila mwisho wa kipengele zitatoa mwanzo bora, hususani kama zimewekewa tarehe.

Hatua za utekelezaji zilizoko katika **Sehemu ya 6** ni muhimu katika kuimarisha ufuatiliaji na utathmini unaofuata. Rekodi haya na tarehe na wakati wa hatua unaotarajiwa. Fanya mapitio ya maendeleo mwaka mmoja au miwili baadaye kukadiria ufanisi wa mbinu mpya za riziki.



*Uuzaji wa matunda yanayoweza kuharibika kwa haraka kama vile, papai kunahitaji mauzo ya juu ili kupata faida. (Picha: Debora Randall / Samaritan's Purse)*

## ZIADA A

# Masomo ya Biblia

Kuna vifungu vingi mno vya Biblia vinavyo husiana na lenzi ya riziki/maisha, ambavyo vinaweza kuwasaidia watu kupata uelewa na msukumo. Sehemu hii ya ziada inajumuisha masomo kadhaa ya Biblia ambayo yanaweza kutumika katika mafundisho ya mwongozo huu kuambatana na vipengele tofauti.

## 1 Maelezo ya jumla ya lenzi ya riziki/maisha

### Kufanya kazi kwa pamoja

1.Wakorintho 1:12 inazungumzia jinsi mwili wa binadamu ulivyo na sehemu nyingi. Somo hili pia linaelezea jinsi gani majukumu mengi yatakavyotekelezwa katika jamii iwapo washirika wake watafanya kazi kwa pamoja kama mwili, na wala si kama watu binafsi. Watu walio katika jamii masikini pegine wanahitaji msaada ili kujifunza jinsi ya kutumia talanta na vipawa walivyopewa na hatimaye kujisaidia wenyewe na vile vile kuchangia katika kusaidia jamii.

### Kufikia uwezo wetu wa kweli

Mara nyingi, jamii hupuuza thamani aliyowapa mwenyezi Mungu . Mchango ambao watu hawa wanaweza wakatoa mara nyingi hauthaminiwi. Katika waefeso 2:10 na Wakorintho 12:6-7, tunakumbushwa ya kwamba sote tumeumbwa kwa mfano wa Mungu – wakiwemo walioambukizwa virusi vya ukimwi, na wasio. Sote tumeumbwa na kusudi fulani, tuna kitu cha thamani cha kutoa. Mungu hana ubaguzi, binadamu anaweza kubagua, lakini Mungu habagui .

Watu walioambukizwa virusi vya ukimwi wana mengi ya kuchangia, iwapo kila mtu, atapata ufunguzi wa uelewa na fursa ya kutoa mchango wake. Tafakari jinsi tutakavyowahimiza wanaoishi na ukimwi kutumia vipawa, au rasilimali ambazo Mungu amewapa.je, ni mambo yapi katika jamii yetu na utamaduni wetu yanayoleta ugumu kwa watu wanaoishi na ukimwi kufikia uwezo wao kamili? Je, tunaweza kufanya nini ili kuboresha hali hii?

### Kujenga juu ya kile Mungu ametupa

Kama vile alivyosema Nehemia na wenzake walipokuwa wanajenga ukuta wa yerusalemu; "Mungu wa mbinguni atatupa ufanisi; kwa hiyo sisi watumishi wake tutaamka na kujenga." (Nehemia 2:20)

## 2 Kuthamini mali

### Kutumia talanta zetu na vipawa

Katika mfano wa talanta (Mathayo 25:14-30), bwana alikasirishwa na mtumishi ambaye alizika talanta aliyokuwa ametunukiwa, ila aliwasifu watumishi wengine waliotumia talanta zao kwa busara. Mfano huu unatuonesha ya kuwa sote tumetunukiwa talanta – ujuzi na uwezo – na tunahitajika kutumia vipawa hivyo. Katika hadithi hii, mtu aliyekuwa na talanta nyingi alitarajiwa kuzitumia vyema, lakini yule aliyekuwa na chache pia alitarajiwa kusonga mbele kadiri ya uwezo wake.

### Waisraeli wasafiri katika nchi ya ahadi

Yoshua 5:10-12. Mungu alitoa chakula kwa mfano wa mana kwa wana wa Israeli walipokuwa wanasafiri jangwani. Hata hivyo, wana wa Israeli walipofika mahali ambapo wanaeweza kujikimu, mana ikaisha. Wakati ukafika wa wao kula na kutumia mazao na matunda ya nchi. Hii inatuonesha kwamba, ingawa kuna wakati wa kupokea msaada, au mbinu ya mahitaji ya msingi, lakini watu na jamii wanahitaji kutazama kile ambacho Mungu amewapa na kuhamia mbinu zinazozingatia maendeleo endelevu kwa kutumia rasilimali.

### Kanuni ya msingi ya rasilimali

Wakati Mungu alipomtuma Adamu kutenda kazi na kutunza bustani (Mwanzo 2:15), Mungu alikuwa anatumia kanuni ya kuzingatia rasilimali kama msingi,kwa maneno mengine, alikuwa anamwambia Adamu aende akatumie kilichokuwepo na kuendelea kufanya dunia mahali pazuri

### Angalia ulichonacho tayari.

Mathayo 14:15-21, Yesu aliwalisha watu elfu tano. Watu hao walikuwa na uhitaji. Walikuwa na njaa, lakini Yesu alipokuwa akishughulikia hitaji lile, alianza na kile walichokuwa nacho wafuasi wake. “Hamna cha kutosha kuwalisha watu hawa wote,” walisema. Naye Yesu akawaambia, “Wapeni watu hawa kitu” wakatoka na wakapata mikate mitano na samaki wawili, naye Yesu akaongeza kile walichokuwa nacho. Mungu anaweza kuzidisha rasilimali zetu, lakini kwanza tunahitajika kutambua ni nini tulichonacho na kuanza nacho.

## 3 Kuelewa mazingira magumu/uathirikaji na mikakati ya kukabiliana nayo

### Kupunguza uathirikaji – Kujenga nyumba juu ya jabali

Katika Mathayo 7:24-27, Yesu alizungumzia juu uathirikaji na uimara. Alisema kwamba wanao yasikia maneno yake na kuyatendea kazi, aliwafananisha na mtu aliyejenga nyumba yakejuu ya mwamba. Mvua kubwa iliponyesha, na mafuriko yakaja, na dhoruba kali ilipovuma na kuigonga nyumba ile nyumba haikuanguka, kwa sababu ilikuwa imara juu ya mwamba. Hata hivyo, Yesu akawafananisha wanao yasikia maneno yake na kutoyafanyia kazi, kama mtu mpumbavu aliyejenga nyumba yake kwenye mchanga. Mvua kubwa iliponyesha, mafuriko yakaja, na dhoruba ikaigonga nyumba ile ikaanguka chini. Nyumba iliyokuwa imejengwa kwenye mchanga haikuwa imara dhidi ya athari, ikaanguka kwa kishindo.

### Kila mmoja wetu ni maalum kwa Mungu

Watu wengi hujihisi kuwa hawawezi. Huenda hawakuweza kuendelea na masomo yao. Huenda walishindwa kutunza familia zao kwa sababu ya ukimwi. Huenda hawajiamini kwa kutokuwa na ufahamu kutoka nje. Huenda walipoteza riziki zao kwa sababu ya janga fulani. Wakati wanapoulizwa maoni yao na wengine, huhisi kuwa hawana chochote cha kushiriki. Ukosefu huu wa kujiamini ni kinyume na mafundisho ya Bibilia hasa yale tunayosoma katika Mathayo 10:29-30 na zaburi 139:13-16. Hapa tunaona jinsi Mungu anavyomthamini kila mmoja wetu. Hakuna mmoja wetu asiye na thamani machoni pa Mungu. Kwa Mungu sisi sote ni muhimu na tunathamani kubwa, licha ya hali zetu.

### Vipaumbele vyetu ni nini?

Mathayo 6:19-24 ni sehemu ya hotuba ya Yesu alipokuwa na Wanafunzi wake mlimani, ambapo Yesu anawaambia wanafunzi wake habari za ufalme wa Mungu. Tafakari kuhusu maana ya kuweka hazina mbinguni. Je, tuna mitazamo inayofaa ili kuanzisha biashara na kupata utajiri?

Kabla hatujaanza kufanya mipango, tunapaswa kuwa na uhakika ya kwamba nia yetu si tu kutengeneza fedha, bali pia kutumia vipawa tulivyotunukiwa na Mungu na kuwabariki walio karibu nasi. Ni vyema kuomba ili tuweze kutumia pesa na mali zetu kwa utukufu wa Mungu, na pia kumwamini Mungu kikamilifu.

## 4 Sera, Taasisi na michakato

### Ustahimilivu katika kudai haki

Katika Luka 18:1-8, tunasikia kuhusu mjane akitafuta haki kuhusiana na mtu aliyekuwa amemkosea. Ingawaje alikuwa na kesi nzuri, mwamuzi alikuwa mvivu na hakutaka kushughulikia kesi hiyo. Alimpuuzia japo mama yule hakukata tamaa. Alizidi kumtembelea hakimu yule akiomba haki. Hatimaye, Ustahimilivu wake ulimshawishi hakimu kuchukua hatua na yule mjane akapata haki.

Mara nyingine, ni rahisi sana kwetu kukata tamaa tunapo puuzwa na walio kwenye mamlaka. Lakini hadithi hii inatupa funzo muhimu kuhusu ustahimilivu.

### Kuwasiliana kikamilifu

Modekai alikuwa mtu mwaminifu na aliyejali. Alikuwa amemtunza binamu yake Esta alipobaki yatima. Alimjulisha kwa mfalme aliyemwoa. Modekai hakutaka kufaidi kutokana na uhusiano wa kifalme aliyokuwanao, lakini alipata maadui wengi, hususani mtu mmoja aliyejulikana kama Hamani aliyetaka kumuua. Hamani alimshawishi mfalme xerxes kutoa amri ya kuwa wayahudi wote wauawe. Katika Esta 4:1-5, tunasoma jinsi Modekai ambaye pia ni myahudi, alivyoingiwa na hofu. Hakuruhusiwa kumtembelea Esta lakini alionesha huzuni yake hadharani, habari hizo zikamfikia Esta. Esta aliposikia hayo aliwatuma watumishi wake kufanya uchunguzi. Kupitia kwao, Modekai alimpasha Esta ujumbe wote, ikiwemo nakala ya amri iliyokuwa imetolewa.

Matendo haya ya ujasiri ya Modekai yalimwezesha Esta kuchukua hatua na akafikisha kesi ya wayahudi mbele ya mfalme xerxes kwa kuchukua hatari binafsi Alisaidiwa kwa maombi na Modekai na wayahudi wengine. Matokeo yake yalifichua hila ya Hamani. (Ni hadithi nzuri inayopasa kusomwa kwa umakini)

### Matokeo ya kupuuza sheria

Hadithi tunayosoma katika Samweli wa pili 13:1-39 ni ya kuhofisha sana, ingawa ni tukio ambalo bado linatokea hata leo hii.Ni hadithi kuhusu kunajisiwa kwa Tamar, msichana mchanga mrembo na shemeji yake(Brother in law) Amnoni. Pia ni hadithi ya jinsi Tamar alivyo telekezwa na wale waliyokuwa karibu naye ambao walistahili kumlinda na kumtafutia haki baada ya kunajisiwa. Hii ni pamoja na watumishi, ndugu zake na baba yake, mfalme Daudi. Daudi hakumwadhibu mwanae kwa sababu ya uaminifu uliogawanyika. Tamar aliambiwa akae kimya. Matokeo yake yaliisambaratisha familia hii.

Hili ni funzo la jinsi ilivyo muhimu kwa kila mmoja kufuata sheria na kutafuta haki wakati maovu yanapotokea.

### Kupanga kwa uangalifu

Nehemia alikuwa mtu mwenye maono makubwa mno! Alitaka kujenga tena ukuta wa yerusalemu wakati wayahudi walipokuwa uhamishoni. Ilikuwa maono yaliyotarajia kurejea kwa wayahudi nyumbani kwao. Nehemia alikuwa mtu

wa matendo na aliyepanga mambo kwa makini. Katika Nehemia 2:1-9 tunasoma jinsi ambavyo alijiweka hatarini mwenyewe,alipokuwa akimwomba mfalme wa babeli ruhusa ya kujenga. Mfalme alimkubalia, sio tu kujenga lakini pia mbao alizohitaji alipewa. Alimpatia barua aliyomkubalia kutenda kazi ile na pia askari wa kumlinda.

Nehemia alipanga vyema na akahakikisha alipata mamlaka ya kuendelea.

# 5 Mzunguko wa thamani

## Kuwa tayari

Katika mithali 31:10-31, tunajifunza kuhusu mwanamke mcha Mungu na mwenye bidii.Mwanamke huyu hukuza mimea, hutunza shamba, hutengeneza malalio na mavazi. Hana hofu ya siku za usoni kwa sababu amejiandaa vizuri. Anaheshimika sana, ana upendo na ni mtunzaji. Mfano ulioje! Tafakari ni nini tunajifunza katika utamaduni wetu, tunapiowaona watu wanaofanya kazi kwa bidii au waliojipanga vyema.Ni nini tunachoweza kujifunza kutoka kwao au kwa mwanamke huyu? Je, tunawezaje kusaidia familia au jamii zetu, ili kujipanga vyema kuhusu siku za baadaye?

## Mtazamo bora wa pesa.

Biblia ina mafundisho mengi mno kuhusu fedha. Biblia haikatazi utengenezaji wa fedha. Paulo alisema kwamba tunapaswa kufanya kazi kwa bidii ili kukimu mahitaji yetu binafsi na ya familia zetu. Katika Timotheo 6:6-12, kuna mafundisho ya busara sana kuhusu haja ya kuridhika na kile tulichonacho na kuwa na mtazamo unaofaa kuhusu mali. Kifungu hiki hakisemi kwamba kutengeneza fedha na kuzitumia vizuri ni vibaya. Ni vyema kutumia uwezo wetu na mali zetu vikamilifu. Hata hivyo, ni vibaya kupenda fedha zaidi ya Mungu. Mtazamo wetu ni muhimu sana katika kujenga biashara.

# 6 Mikakati ya riziki/maisha

## Ushirikiano

Katika Kutoka 17:8-13, tunasoma juu ya mfano wa kutia moyo kuhusu yale tunayoweza kutimiza iwapo tutafanya kazi kwa pamoja kama kikundi. Musa na Yoshua walifuata yale walioelekezwa na Mungu wayafanye. Wakati Musa alipochoka, wenzake walimsaidia na kushirikiana naye katika kubeba mzigo, kwa matokeo bora. Bila ushirikiano huo, uwezekano wa kulemewa au hata kupata janga ungetokea. Tutawezaje kusaidiana kwa kutumia vyema rasilimali tulizonazo? Je, ni watu gani katika jamii yetu wanaweza kutusaidia katika mambo haya?

## Hazina ya mbinguni

Katika Mathayo 6:19-24, Yesu anatuambia kwamba, badala ya kuweka hazina hapa duniani, tuweke mbinguni. Hazina za hapa duniani hazidumu na huenda zikapeleka watu mbali na Mungu. Licha ya kwamba tunaweza kuwa na mali chache tunazomiliki, sote twaweza kuwa matajiri kutokana na hazina ya ufalme wa Mungu, je, kifungu hiki kinatusaidiaje kuona kwamba hatimaye lengo letu sio tu kuweka hazina hapa ulimwenguni, bali kutazamia umilele?

### Ustahimilivu

Kuna furaha kubwa sana katika kuvumilia hadi kukamilisha yale aliyotuitia Mungu kuyafanya. Wote wawili; Yesu na Paulo walitangaza katika mwisho wa maisha yao kwamba wamemaliza majukumu yao. (2 Timotheo 4:6-8, Yohana 4:34, Yohana 19:30). Je, tunafahamu majukumu ambayo Mungu ametupatia – katika familia, kanisa, au jamii? Je, tutaweza kurudia maneno aliyoyasema Yesu? "Nimekuletea utukufu hapa duniani kwa kukamilisha kazi uliyo nipa kuifanya." (Yohana 17:4)

## 7 Kuchukua hatua

### Kuhesabu gharama

Katika Luka 14:25-30, Yesu anatoa mfano wa vitendo kuhusu haja ya kuwa na mpango wa kina. Je, ni nini kinachoweza kutokea kwa mtu anaye anza ujenzi bila kukadiria gharama yake kwa jumla? Umezingatia kwa makini rasilimali zote (kama vile fedha, wakati, na afya) ambazo zitahitajika kwa riziki unazozingatia? Je, una mipango mingine, iwapo huna uhakika wa kufaulu? Je, unaamini gharama ya kumfuata Yesu ina thamani ya kulipwa? hii ina maana gani kwa maisha yetu ya kila siku?

### Kuwapata watu wa kukusaidia panapohitajika

Katika kanisa la awali, wayahudi wa kigiriki hawakufurahi kama tunavyojifunza kutoka Matendo ya mitume 6:1-7. Walihisi kwamba wajane wao walikuwa wamepuuzwa. Wafuasi wa Yesu walikuwa makini kusikiliza na kuchukua hatua. Pia walifanya maamuzi ya busara kutafuta msaada kushughulikia swala hilo badala ya kulitatua wenyewe na kuwa na muda mchache wa kushiriki neno la Mungu. Walitafuta watu waliojazwa "Roho mtakatifu na hekima". Kufuatana na haya, swala lile lilitatuliwa, na kanisa likakua kwa kasi sana. Huu ni mfano bora wa kushughulikia matatizo, na haja ya uwepo wa msaada zaidi. Ni vyema kuajiri watu kufanya majukumu tofauti kulingana na vipawa vyao na ujuzi na upako wa Mungu juu yao.

### Matumaini katika hali yoyote

Sisi sote twaota ndoto mara nyingi. Kuna mambo ambayo tunatarijia, lakini mara nyingine huonekana kama haiwezekani kuyafikia. Tunakosa Matumaini na tunahisi kwamba hatuwezi kubadili hali tuliyonayo. Ukisoma Warumi 5:1-11., utaona jinsi hali ya kukatisha tamaa inavyobadilishwa na upendo wa Mungu unao dhihirishwa kwetu kupitia kifo cha mwanae. Aya ya 3 na 4 inazungumzia kuhusu kujivunia magumu yetu! Je, umewahi kuona upendo wa Mungu na mafunzo yake kupitia mambo magumu uliopitia? Je, umewahi kushuhudia upendo wa Mungu kupitia mateso?. Ukisoma aya 10 utaona inavyotupa faraja.

### Kuangalia matatizo kwa kutumia macho ya Yesu


Ukisoma Yohana 6: 5-15, kifungu hiki kinatukumbusha Yesu alipokuwa akikumbana na magumu mwanzoni mwa huduma yake lakini aliyashinda. Wafuasi wa Yesu hawakujua jinsi ya kulisha umati mkubwa, lakini Yesu alichukua rasilimali kidogo waliokuwa nayo tayari – mikate mitano na samaki wawili na akazidisha. Sisi pia huenda tukapata hali au mambo yasiyowezekana lakini hadithi hii inatufundisha kuanza na kile tulichonacho hata kama ni kidogo. Yesu hutusaidia kuzidisha rasilimali zetu iwapo tutaziweka katika matendo.

# Kutumia hadithi za Biblia kufundishia kikundi

Unaweza ukatumia mafundisho yoyote kati ya haya katika makundi madogo ya kusoma Biblia wakati wa mafundisho, kwa kuuliza maswali yatakayo wawezesha watu kutafakari na kujifunza kutoka kwenye vifungu hivi. Watu wasome vifungu kwa pamoja katika makundi madogo ya watu watatu au wanne, na uandike maswali tofauti ya kila kikundi.(Katika kikundi kikubwa,unaweza ukatoa maswali yale yale kwa makundi mawili au zaidi) buni maswali yatakayowafanya watu kufikiri wenyewe – Uliza kuhusu historia ya hadithi, nini kilifanyika, ni nini wanachoweza kufanya wakawa katika hali kama ile na ni mafunzo gani tunapata kutokana na hadithi hiyo leo hii. Kisha walete watu pamoja na uwaulize wabadilishane majibu (Kwa mpangilio wa maswali)

Hapa kuna mfano wa jinsi ya kufanya kwa kutumia hadithi iliyo hapo juu.

## Kuangalia matatizo kupitia macho ya Yesu



Ukisoma Yohana 6:5-15. Utaona Yesu akipitia magumu wakati akianza huduma lakini baadaye alishinda nasi twaweza kushinda.

1. Ni hali gani inayoelezewa katika kifungu hiki? Ni tatizo gani alikumbana nalo Yesu na wafuasi wake?
2. Filipo alijibu vipi? Yesu alilijua jibu hata kabla ya kumuuliza Filipo swali, je, kwa nini akamuuliza?
3. Iwapo tungekumbana na hali kama ile, tungekuwa na jibu tofauti na lile la Filipo? Sisi twakabilianaje na changamoto maishani mwetu?
4. Kuna mafunzo gani tunayoweza kupata kutokana na hadithi hii?

Uwezekano wa majibu ni kama haya.

1. Umati mkubwa ulivutiwa na Yesu kwa sababu ya uwezo wake wa kufunza, lakini kule mashambani, mbali na miji ingelikuwa vigumu kupata chakula cha kutosha kuwalisha wote – hata kama wanafunzi wangelikuwa na fedha za kutosha.
2. Yesu alitaka kumjaribu Filipo. Vile vile, Yesu anaweza kutuletea hali ngumu zinazo onekana haziwezekani – kutujaribu na kujenga imani/matumaini yetu. Mungu anataka tuelewe upendo wake. Mara nyingi tutajiona wadogo mno tunapo tazama hali na changamoto za duniani.
3. Pengine tungelifanya kama Filipo lakini imani yetu yapaswa kutupatia uelewa (insights) zaidi. Hatufai kutizama matatizo kulingana na uwezo wetu.
4. Yesu alitumia kitu ambacho watu na wafuasi wake walikuwa nacho mikononi mwao. Alitaka kuwafundisha wanafunzi wake. Alitaka wawe na juhudi kidogo. Chochote kilichopo, kinaweza kutumika. Yesu anataka tukue, anataka kubadilisha mioyo yetu.

**HITIMISHO:** kama jinsi mbinu hii ya lenzi ya riziki, Yesu anauliza watu wajihoji nafsi zao ili kutafuta kidogo kilichopo – katika misingi ya rasilimali na ujuzi. Kitaongezeka iwapo kitawekwa katika matumizi.

**Usitufanye tugeze matatizo au changamoto kulingana na uwezo wetu au vikwazo.**

## ZIADA B

# Masomo zaidi


Brown S et al (2006) *Livelihood strategies in the rural Kenyan highlands.* World Vision

CARE International (2009) *Mapping vulnerability profiles of low capacity households*. www.careinternational.org.uk/research-centre/governance/49-mapping-vulnerability-profiles-of-low-capacity-households

Catholic Relief Services: *Integral human development: the concept and framework* at: www.crsprogramquality.org/IHD/

Catholic Relief Services / USAID (2008) *Agriculture and environment interventions in support of HIV programming*

Dazé A et al (2009) *Climate vulnerability and capacity analysis handbook*. CARE www.careclimatechange.org

Department for International Development (DFID) *Sustainable livelihood guidance sheets* www.eldis.org/go/topics/dossiers/livelihoods-connect/what-are-livelihoods-approaches/training-and-learning-materials

Eldis Livelihoods Connect website: www.eldis.org/go/livelihoods/

International Fund for Agricultural Development (IFAD): www.ifad.org/sla/framework/

Mayoux L (2005) *Participatory action learning system* http://lindaswebs.org.uk/Page3_Orglearning/PALS/PALSIntro.htm

Tearfund publications: *Footsteps*, *ROOTS* and *PILLARS Guides* http://tilz.tearfund.org/Publications/

The HIV Alliance (2006) *Tools together now – 100 participatory tools to mobilize communities for HIV/AIDS*

## ZIADA C

# Michoro ya Rasilimali

Tolesha nakala za kurasa hizi nane na kisha baadae uikate michoro yote. Waulize washiriki waipange kwa aina yao katika makundi sahihi (ona zoezi katika ukurasa wa 17) na kisha watambue mali husika kwa wenyewe.




Ujuzi wa kupika



Ujuzi wa kujenga



Juzi wa kukarabati baskeli



Ujuzi wa kurekebisha mitambo




Ujuzi wa kushona



Ujuzi wa useremala



Kujua kusoma na kuandika




Kusoma shuleni



Sifa za kuhitimu




Hekima



Maono ya usoni



Nguvu



Bibilia



Kanisa



Mahubiri




Ushirika



Maombi



Matumaini




Marafiki



Vikundi vya chama




Watunzaji wa nyumbani




Familia



Vikundi vyawakulima




Kundi la kuhudumia wanaoishi na VVU




Zahanati



Kushiriki katika harakati za kufanya maamuzi




Usajili wa ardhi




Mfumo wa sheria




Polisi




Haki ya kupiga kura





Mashirika yasio ya kiserikali



Viongozi wa mtaa




Wazee/Machifu





Haki za kibinadamu





Nyumba



Vifaa vya ukulima



Vifaa vya useremala



Runinga/Televisheni


Kamera


Tarakilishi/Kompyuta


Radio



Gari


Piki piki



Baskeli




Mifugo – kuku




Mimea – Nafaka




Mimea – mandizi



Magunia ya nafaka yaliohifadhiwa




Fedha





Benki




Kundi la hazina




Shirika ndogo la kifedha



Maduka na hifadhi




Soko




Miti na mbao




Vyanzo vya maji



Samaki



Ardhi




Mito



Jua




Majabali na vifaa vya ujenzi




Mimea ya msitu



Udongo



Wanyama wa msituni



Nyuki

**Rasilimali za kibinadamu/ Kiroho**

**Rasilimali za kijamii**

**Rasilimali ya kisiasa**

**Rasilimali za kiumbo**

**Rasilimali za kifedha**

**Rasilimali za asili**

## Vidokezo

# Fikiri riziki!

Mwongozo wa wawezeshi wa kutekeleza lenzi ya riziki ukifanya kazi na watu, familia na jamii zilizoathiriwa na virusi vya ukimwi.

Tafsiriwa kutoka **Think Livelihoods!**
Chapisho la pamoja la…

Tearfund
**www.tearfund.org**
100 Church Road, Teddington, TW11 8QE, UK
Tel: +44 (0)20 8977 9144

Nambari ya usajili (Nchini uingereza na wales)
Nambari ya usajili (Nchini Scotland)

20770 (0512)

Samaritan’s Purse, UK
**www.samaritans-purse.org.uk**
Victoria House, Victoria Road, Buckhurst Hill
Essex, IG9 5EX, UK
Tel: +44 (0)20 8559 2044

Nambari ya usajili (Nchini uingereza na wales)
Nambari ya usajili (Nchini Scotland)